Finally, the right of ownership - if a man impregnates a disabled person he should be forced to take both the mother and the child.

Parents with disabled children should not hide them but instead expose them so that the government will assist them.

Com. Kangu: If you have a written memorandum, why don't you just highlight.

Mrs. Mutisya: I am now getting to finish.

Com. Kangu: You are finalizing, fine.

Mrs. Mutisya: Wife beating should be abolished. Dowry must be enforced and especially the three goats in kamba culture should be paid.

I am now at the disabled people. Public buildings should have facilities for the disabled people. They should be given special

attention in the employment sector. They should be given opportunities in higher offices.

Child rights - children should be given basic needs. The government should consider the fate of street children and help them stop becoming mothers on the streets. Grandparents of orphans should be assisted by the government to bring up the orphans. They should be provided with land. Rape victims especially minors should be given attention. Both parents should be involved in bringing up children otherwise be prosecuted. All the Kenyans should be getting an automatic allowance at least Kenya shillings 300 per head after a period of thirty days for those who are not employed to cater for themselves. That is all.

Com. Kangu: Thank you.

Com. Maranga: There is one question I wanted to ask, it might be interesting. You have said no wife beating, but do you know there is also husband beating.

Mrs. Mutisya: That one I was talking of women, I was not talking of men. I was not talking of the husbands.

Com. Ayonga: In other words you would like to see husbands being beaten but no wife beating.

Mrs. Mutisya: But that one doesn't occur very much.

Com. Ayonga: Why don't you want to say, that no beating of any person, spouses because many men are being beaten and they are ashamed to say. Now, I have a question, a small question for you, you said that nomination seats should be reserved for women and disabled. Now, did you know also that women are 52% of the Kenyan population and they are so many, that if they wanted to bring it to Parliament or to the councils their women folk that they will do it, why should many people need reserved seats when they can take the actual seats because of numerical number? And doesn't this weaken the woman further that she cannot do her campaign unless you give her a seat. You want to be given seats in a platter?

Mrs. Mutisya: You know of late we women we have not been able to go to Parliament so that is why I was talking on behalf of them, so that if we don't get chances then we can be nominated this time.

Com. Ayonga: Can't you fight yourself?

Mrs. Mutisya: We will fight.

Com. Kangu: Let us hear mama Phoebe.

Com. Asiyu: Two questions, one on the same issue. You are aware that there are countries in this sub-region like Uganda, Tanzania, maybe in South Africa, Namibia and others who have special arrangements for women to be elected to both local authorities and Parliament by holding elections for women representatives only at the district level, so that every district will have one woman elected by the people on a political party ticket. That in this country will give women like 74 members of Parliament to start off with.

Then strong women who can face up with the men like Ngilu and others can also stand and compete alongside with men. You have not made such a recommendation. I want to know from you, that is what they call affirmative action in those countries and you also know that women in Kenya have really fought for that affirmative action to be implemented either at the district level or any other level that will be acceptable and that they have been brought back now to this Commission.

I want you to tell us because you are representing over one million women in this country, those with the membership of the maendeleo ya wanawake. Tell us whether you support this practice of affirmative action as it is done by our neighbouring countries or whether you prefer that women be nominated the way you have suggested.

Number two, you have told us that a woman should be able to inherit from her father's property but when she gets married, that property should be reverted to the father's home. Now if supposing this woman had put up a building in that area, the piece of land that was given like a shop or if it is an apartment as a business, or even a piece of land which she will then cultivate and supposing she got married to a man who does not have any land, would you still suggest that this property be reverted back to her brothers when she has nothing in the home where she belongs?

Mrs. Mutisya: I will first answer the first one, you know we women in-let's say in the local area, we are not very aware of whether that formation of other countries has been formed and this is the high time now we are knowing. So we will very much support that one for other countries that women should be enlightened to know that there should be a formation of that nomination. I would rather support that one.

The second one, you asked me about the land. That one I would rather say, whereby a woman has been married then the land should go back to the parents.

Com. Asiyu: If it is not possible to go back to the parents but where for example she has put up a building on a piece of land given to her by her father. Originally there was land, would she leave it to her brothers. Are you suggesting that she should leave this investment to her brother?

Mrs. Mutisya: Whereby the land had not been transferred to her, officially transferred to her she will leave it but not to be forced. If she wishes but if she doesn't wish she should not be forced.

Com. Kangu: May be there are issues you need to go and think about and if you want to do a personal memorandum you prepare and send to us. Thank you, sign and hand over the memorandum there. Can we now have George Ogutu a civil servant.

Mr. Ogutu: Thank you Mr. Chairman, the Commissioners, bwana D.O, teachers and students of Kathiani High School, my names are George Ogada Ogutu. I want to dwell on just two issues here.

First I want to talk about the crime rates in our country which affects everybody. I think everybody knows that right now at this moment crime rate is bothering every citizen of this country and my request was just to tell the Commissioner to look for a way of making members of the public enlightened about their own rights concerning the law of this country.

Very few people mostly in the rural areas don't know their rights according to the law as far as law is concerned and that is why the crime rate in the country has escalated to the current trend.

I want to tell the Commission to make it mandatory if it is possible for parents to account for the movement of their kids or their children. Parents should be compelled to register the behaviour of their kids because they are the ones who know the behaviours of their kids from their childhood.

They should also be compelled to ask for the wealth of their kids. If you have a son and he is not working na ni tajiri sana anatoa pesa wapi, ako na magari wewe humuulizi hushughuliki why? You should also be concerned. Ukikataa hiyo you encouraging crime. You must be compelled to ... if anything goes wrong you will also be held responsible if you cannot disclose the movement or the character of your kids.

Com. Kangu: You try and move fast.

Mr. Ogutu: I have done away with the crime and now I want to talk on politics. At the moment sheria inasema ya kwamba the winning Presidential candidate anakuwa determined na the number of votes he gathers in the general elections. I would propose that the winning Presidential candidate should be determined by the number of seats his party gathers.

The reason why I am saying this is because this will discourage this issue of numerical number ya ukabila na nini. It will also discourage the issue of defection from one party to another and it will make us more cohesive than we are now because I believe a nation should be a united nation, not a nation which is disunited kwa sababu ya misingi ya kikabila.

Ya tatu, ni kuhusu land - Land policy should be looked into. We have so many people with huge tracks of land, which are

undeveloped. Some are bushy and are being used as hide outs for criminals and wild beasts even in my rural areas where we have leopards what, let's us say hyenas but if people can be compelled to surrender the extra land that they have if they can't develop the land to others who don't have or we have a clear policy on land issue the better. I think I will stop there.

Com. Kangu: Thank you very much. Sign our register, can we have Mary Charles from Maendeleo. Mary Charles, ni wewe? Kama hayuko, tupate Florence Maithya, kama hayuko tupate John Nzioki Muli, ni wewe? Please take a seat. Wewe ndio unaitwa nana mama? Mary Charles, take the seat lakini unakaa hapa kama unaandika jina unaenda nje itakuwa mbaya. Taja majina na uanze kuzungumza mambo yako.

Mary Charles: Kwa majina ni Mary Charles. The chairman for this meeting, the Commissioners and all the participants, ladies and gentlemen. Ningelipenda nizungumze kwa kiswahili.

Com. Kangu: Sawa sawa.

Mary: Mimi ni secretary wa Maendeleo ya Wanawake Kathiani. Niko pamoja na yule amesoma maneno ya ile memorandum ya wanawake. Kwa hivyo individually ningependa tu niongeze machache. Kwanza ningelipenda niulize Commission ichunguze sana juu ya sisi wanawake. Wanawake watoto, wanawake wazima, wanawake wazee, huku pande ya rural area. Sisi huwa na taabu nyingi sana ambazo huwa hazijulikani na ningependelea sana mambo yetu yachunguzwe sana ikiwa tungependekana tuwe tunaishi kama watu

Tena ningependa niulize Commission kama ingeweza kuchunguza mambo ambayo yanatoka pesa zetu, tuseme tukiwa huku reserve sisi huwa na taabu nyingi sana ambazo ikiwa tuseme for example huku sana sisi tunajisaidia na pesa za kahawa, kahawa siku hizi hatuna pesa kutoka kwa kahawa. Imejaa kwa mashamba, hakuna pesa zinatoka kwa kahawa, tunajisaidia kusomesha watoto na hizo pesa na pia kujisaidia mambo ya kibinadamu. Tungeuliza Commission ichunguze sana juu ya kahawa, sisi imefika kiwango ya kuona haina maana hata kidogo kuwa kwa mashamba yetu kwa sababu tuna shida ya pesa na hiyo kahawa haitupatii pesa. Why? Kwa sababu wale watu wako juu pale wanakula hizo pesa, hatuzipati sisi. Kwa hivyo tungeomba Commission iangalie hiyo sana.

Pia, ningepomba Commission ichunguze sana juu ya shule ambazo ziko huku reserve. Mapato ya watu ambao wanaishi reserve ni machache sana na ikiwa mzazi hata kama anataka kusomesha na mapato yake hayako watoto, elimu ya watoto inakuwa shida sana ingawaje wanapenda kusomesha.

Kwa hivyo ningeponelea ni vizuri ili Commission iangalie hayo mambo ya shule za huku ikiwa ingeweza kutofautishana na zile za town ndio watoto wa huku reserve wapate elimu. Pia, ningepomba Commission ikiwa ingeweza kutengeneza upya mambo ya masikizano nyumbani. Sisi watu wa reserve kwa sababu wengi wetu hatujui kusoma sana sana wanawake tuna shida sana

tunapoishi na waume wetu. Sio kwamba ni wabaya ni kwa vile imekuwa hivyo na ikawa ni kama mtindo wa huku anaonelea haina maana kunijulisha mambo ambayo yanahusu for example kama land, yaani hata property tuseme properties zile ambazo mtu angepaswa kuwa nazo na kwa hivyo inakuwa ni ngumu sana kwa wanawake ikiwa kwa mfano bwanake amefariki, huyu mama anateseka sana kuchunguza kutafuta mali ya bwanake, hiyo tunaonelea sio vizuri. Na kungekuweco maandishi ya kuonyesha huyu mama anajua mahali iko, ingekuwa rahisi kujua mali yao. Kwa hivyo ningepomba Commission iangalie hiyo upya.

Naomba tena Commission ichunguze tena ikiwa kungeweza kuwa wakituma watu kwa shule za huku kutuma watu ambao wangukuja wazungumze sana na watoto kwa sababu shule za huku watoto wengi wanaweza kufanya makosa kwa sababu ya kutokujua. Sasa unajua ikiwa ni waalimu wako na kazi nyingi sana ya kusomesha watoto. Sasa tungeomba Commission ipange mpango wa kila shule huku reserve na kwingineko kuwe na Councillors wanakuja shule ili watoto wawe, yaani licha na masomo yale wanasomeshwa na mwalimu awe mtu anajielewa mwenyewe. Kwa hivyo ningeponelea ya kwamba upande huo ningesema hayo nikuongeza tu nilikuwa naongeza yale yamesemwa tu, tuko pamoja na wale wameandika na ningeponelea nitapendekeza ili tuwe hatuishi vibaya ikiwa tutapata Serikali ingine.

Com. Kangu: Thank you umemaliza ee? Asante just sign our book tupate Florence Maithya.

Mrs. Maithya: I am Florence Maithya na nitaongea na kiswahili ndio akina mama walioko nyuma ambao hawaelewi Kiingereza ndio tuelewane. Yangu ni kuzungumza juu ya akina mama kwa sababu yule chairlady tulikuwa pamoja tukiandika ile memorandum, yangu ilikuwa pamoja na hiyo ya chairlady lakini nitaongeza kitu kidogo kwa sababu wale akina mama tumeandika ile ilikuwa ni yetu kwa upande wa akina mama.

Kwa kawaida akina mama wetu wako na taabu kinyumba, wanawake kwa upande wa akina mama wanaume wengine wameacha nyumba zao na kuondoka, kwa hivyo akina mama wameachiwa kazi ngumu ya kinyumba na ndio ikaingilia kwa upande wa groups zikaingia ndio zianze kusaidiana. Kwa hivyo ningepomba kama wanaume kama wangeshikana pamoja na akina mama kama vile groups zimeingiana kama akina mama wameshikana pamoja. Sasa wanaume wangukuwa na groups kama akina mama nchi yetu ya Kenya ingekuwa imeendelea sana kwa sababu akina mama ukiangalia ndio wamevuruta maendeleo sana na wanguungwa mkono ni wanaume wao ili kwa mila zetu ingekuwa juu sana. Kwa hivyo ningepomba kamishina sijui kama wanaume wanguweza kuwa na seminars ndio wafuate akina mama wetu, ndio wawe na mwongozo mmoja ndio tuwe na maendeleo yetu. Ie ingine imesemwa ni chairlady wetu ilikuwa ni ya wasichana wetu na kwa sababu amesoma ningeponelea kwa upande wangu niachilie hapo kwa sababu mambo yetu ile tulikuwa nayo imesoma hapo. Na hatuna mengine.

Com. Kangu: Basi sign our book, na kama hatujaendelea I would like to recognize the arrival and presence of the area Member of Parliament Hon. Kaindi, bwana Kaindi welcome tuko kwako na tutakupatia nafasi baadaye kuzungumza tunataka kwanza usikize mambo ya watu wako kidogo na wewe utazungumza baadaye. Let's move to the next person John Nzioki Muli.

Mr. Muli: Kwa chairman wa Commission na Hon. Na wengine na raia wenzangu. Majina yangu ni John Nzioki Muli na mambo yale nilikuwa ningesema nimeandika...

Com. Kangu: Kama umeandika you just highlight halafu Utatupatia memorandum or if you want to give us just the memorandum and add nothing it will be up to you to tell us.

Mr. Muli: Nimeandika na nilikuwa nataka kupeana kwa hivyo sitasoma.

Com. Kangu: Peana pale na uweke sahihi. Na sasa tupate Ruth Mwasya from Maendeleo ya Wanawake.

Ruth: Asante sana bwana chairman. Yetu ilikuwa ile imesomwa hapa na chairlady lakini nataka kuongeza kitu kidogo hapo. Sisi wanawake wa huko nyumbani ama watu wa rural areas kama ingewezekana tuletewe stima kwa kila nyumba kwa sababu mnajua miti siku hizi ni ndogo, michache na hakuna miti. Tunataabika sana akina mama kwa kupika hata kwa kuona hakuna mataa. Tungeomba Commission itupatie stima.

Tena, tungeomba kama ingewezekana tujengewe barabara nzuri kwa sababu sisi akina mama tukiwa na mgonjwa tunabeba kwa mguu kwenda hospitalini, hakuna barabara nzuri.

Kile kingine tunataabika sana tukiwa kwa mazao yetu, huko rural areas hakuna mpango mzuri wa kujipatia pesa za kujisaidia. Na kile kingine naweza kuongeza kwa ile ilisomwa ni kuhusu wasichana wadogo. Tungeomba Commission kama ingewezekana wachunguze sana wale watu wana-rape watoto wachanga, wawe wanapewa hukumu ile inawezekana kwa sababu mtu anafanya kitendo kile anaona ni cha kinyama kwa mtoto, kwa hayo yote asante.

Com. Kangu: Asante basi. Nenda uweke sahihi pale mama. Tupate Anna Munyao from CBD.

Anna: Kwa majina mimi naitwa Anna. Yetu ilikuwa imesemwa na mwandishi wetu wa Maendeleo ya Wanawake. Ya kuongeza, sisi siku hizi wanawake tuko na taabu, kwa sababu wale wanawake wanaoendesha ya biashara hakuna barabara nzuri. Wanabeba mizigo na mgongo mtu akitoka hapa anaelekea Machakos mgongo anapeleka vitu vyake huko.

Kile kingine, wale wazazi wanazaa siku hizi tuko hatarini sana. Hakuna pesa, hakuna kitu ya kujisaidia. Kujisaidia mvua ile iko mwaka huu ni mvua inayoonyesha ni nzuri lakini wakati mwingine mvua hakuna. Kazi ya wanaume ya hakuna, ni kibarua tu. Wanawake wa siku hizi tuko hatarini sana. Watoto wa shule saa yote unaona wanafukuzwa, hakuna kile kitu wanaitishwa na mwalimu. Masomo siku hizi ni ngumu, kile kingine naongeza hapo ukiona watoto, wengine wako na nguo mbaya na fee ya

mtoto ni mzazi, hakuna kitu. Tukilima hakuna shamba.

Siku hizi, mwaka huu kuna mvua tunapata chakula kidogo. Ni hayo tu.

Com. Kangu: Ni hayo tu. Asante sana. Kuna swali moja mama, ngoja.

Com. Asiyu: Umetueleza shida ya akina mama na pia umetueleza shida ya watoto kwa ajili ya umaskini yaani hakuna mapato, kama hakuna mvua wanaume hawana kazi. Lakini ungetuambia unataka tuandike pendekezo gani kwa Katiba. Kama ni mambo ya watoto, ungependa kwa mfano tuseme kuwe na elimu ya bure kutoka class one mpaka kiwango fulani ili wale wazazi maskini pia watoto wao waende shule.

Pili, ungependa kusema nini juu ya ukosefu wa kazi. Unaona ni njia gani nchi hii inaweza kujiendesha kwa kupata kazi kwa wale wanaume wasio na kazi.

Anna: Serikali isaidie.

Com. Asiyu: Kwa mambo gani? Umesema jambo moja.

Anna: Tupatiwe elimu ya bure kutoka std. One, two, three, four kufika eight.

Com. Asiyu: Kufika class mne peke yake?

Anna: Kufika eight.

Com. Asiyu: Na mambo ya umaskini ifanywe namna gani?

Anna: Mambo ya umaskini hiyo ni moja ya kumaliza umaskini kwa sababu kuna wamama hawana kitu na hakuna kazi na mtu anataka kusomesha watoto,

Com. Asiyu: Hiyo tumesikia, sasa wewe upendekeze Katiba iseme namna gani?

Anna: Katiba iseme watu wasaidiwe. Sijui watasaidiwa na nini. Kwa ni kisomo tu cha bure.

Com. Asiyu: Na tumefahamu basi asante sana.

Com. Kangu: Asante mama wewe umepeana maoni vizuri, unasema Katiba iangalie uchumi uwe mzuri, sawa sawa? Nenda uweke sahihi na kuna mama Dorothy Kiilu wa maendeleo. I hope hakuna mambo mingi ya kuongeza.

Dorothy: Mimi naitwa Dorothy Kiilo wa Maendeleo ya Wanawake. Commissioner nataka kuongeza kitu kidogo tu lakini yale mengi yamesemwa. Sisi wanawake tuko na taabu. Tunataka ututetee ukirudi huko. Wanaume tunakaa nao kwa nyumba na mtu hataki kwenda kufanya kazi na wewe mama unajua pahali unaweza kuenda ufanye kazi kidogo upate pesa ili uje utolee mtoto fees. Naye anaku-damp kwa nyumba, hataki kukupatia ruhusa ya kwenda ufanye kabiashara ili upate kitu, anataka mukae hapo tu. Tunataka Commissioner ukienda huko hata ikiwa ni seminar ya kuwekea wanaume ambao wako kichwa yao iko chini, hawataki maendeleo, uwafundishe ili tutoe umaskini kwa nyumba. Yangu ya imefikia hapo. Asante.

Com. Kangu: Tunyamaze tumsikize mwingine, mama amesema mambo ya muhimu. Kusema kweli ukienda rural areas mara mingi wanaume hawataki kufanya kazi, ni kuondoka kwenda kutembea jioni wanarudi wanataka chakula kama hakuna wanapiga mama na najua haya mmesikia. Si ni kweli? Basi tumsikize chief Charles M. Ngalama. Yuko ama hapana? Kuja tu uzungumze bwana chief hata na wewe uko na maneno ya kutueleza.

Com. Maranga: Hapana ogopa D.O, pengine anaogopa D.O.

Com. Kangu: D.O hana shida, wewe kuja uzungumze maneno yako, huu ni mkutano wetu. Basi kama hataki basi tumsikize assistant chief James K. Muzee. Hata na yeye hapana taka? Basi wacha niwaeleze hivi, sheria tunayo yenye tunapata inasema yeyote mkenya ako ruhusa kupeana maoni yake, hata D.O akitaka kupeana maoni yake atatueleza. Anatayarisha na hiyo sheria tena inasema, ikiwa kuna mtu yeyote hataki kutoa maoni mbele ya watu anataka tumsikize kando peke yake tutamruhusu sasa bwana chief, bwana assistant chief ikiwa unataka tukusikize in camera utueleze tutakusikiza because we want to hear views from everybody si ni kweli?

Na kama unataka kupeana written memorandum, utapeana. Jana tulikuwa muuma andu na tulisikiza mpaka tu five chiefs and assistant chiefs wakatupatia maoni ya muhimu sana. Kwa sababu kuna wale wanakuja wanatuambia hawa watu wote toa, lakini nyinyi mko with the story of the other side. You must tell us na msipokuja kutuambia we may not know the other side of the story, tunaielewana? Basi tusonge kwa wengine watafikiria watatuambia baadaye. Paul K. Makau. Pia yeye ni assistant chief, Alice Nduku, chairlady KANU, basi songa mbele.

Alice Nduku: Kwa majina naitwa Alice Nduku na mimi ni chairlady wa sub-location kutoka Ngoleni, KANU. Sisi wamama tuko na shida wakati wa kulea watoto. Shida zetu ni tunaposomesha wasichana wetu unaweza kumpeleka kwa shule na pengine umetafuta karo kwa shida na akimaliza mwaka mmoja anachukua mimba, anazaa mtoto ile shule amekoma kuenda shule, anakuja anazaa, unamuonya usirudie haya nitatunza huyu mtoto, utarudi shule. Huyu mtoto, yule alimtungua mimba anamnyemelea tena, anamueka ingine.

Mimi nasema hawa watu kwa sababu hawana heshima na ndivyo wafunzwe vile wanaweza kukaa, maana wanaongeza shida kwa nyumba na huyo kijana hana nguvu za kumuoa huyo msichana, anampea watoto kama wawili na anamuacha. Sasa inakubidi kuwa na shida, inaendelea nyumbani. Sasa nauliza kama inawezekana kutafutwe adhabu ya hao watu wawili. Wakionywa ikiwa hawaoani, wafungwe ama wapewe adhabu kwa sababu wanazaa watoto na wanawaacha hivyo, mtoto hana baba, na ana mama na hana msaidizi mwingine. Sasa itakuwa shida kwa nyanya yake kwa kuwa anakuwa na mzigo mkubwa. Kwa hivyo hawa watu wawili wachukuliwe hatua ili waonyeshwe haya ni makosa kufanya hii na hawaoani na hawana kitu, hii ni kufanya nchi yetu iendelee kuwa na chokoraa hawa na kwa hivyo naomba Serikali ichukue hii kama sheria moja ili kuwatunza watoto hawa wa aina hiyo. Kwa hivyo maneno yangu ni hayo nakoma hapo.

Com. Kangu: Asante basi weka sahihi kwa kitabu na kuna mwalimu kutoka Kathiani Girls na students tulikuwa tumewaita mapema walikuwa hawajaingia nasikia sasa wamerudi. Wa kwanza alikuwa Lillian Awuor, mwanafunzi, yuko?

Lillian Awuor: I am Lillian Awuor from Kathiani Girls and these are some of the views we would like to propose as students. First, there is brain drain in the society, that is you get a person learning for more than ten years you go to school after university, then there is a man who is over 80 years, he still has the job while you are young, you got a family and you can't provide for their needs because you don't have a job while that guy who is over 80 or 90 years still working and has the job.

The second one is institutional discrimination. These are some of the problems we face in schools such as this one because you get a person or a student ...

(Interjection)

Com. Kangu: Use the mic so that we can hear well.

Awuor: A student from a school like Kathiani Girls does the exams and passes, maybe he gets a A- and then another student from a famous school like precious blood or those national schools, once you go to the higher level education of the person who has that C- or C+ because she was in a better school than yours has higher chances of getting an opportunity while you have done better than her.

We were suggesting for fair salaries in the society. Here we were suggesting that people should be paid the labourers should be paid according to the number of hours they work. The sum of labourers who do very less in the society while they are the most paid while those who do a lot of work like teachers in the society they are lowly paid.

Fourthly, freedom of the press - The press doesn't have freedom to express their views in a way, they are restricted in some ways, in that you find that the journalists are treated harshly, other times they may print a story about those big guys and then

they are sued because they are trying to interfere with their private life. How are we to know how our leaders are if we only see them as those dictators we see them in television when they come they say you should do this and don't do that, while we don't know their social life and then patriotism:

Like in our country, our leaders always tell us to be patriotic to our country while they themselves have other investments outside the country, it is not bad well but if they could have invested in our country I guess we could be more rich and then they expect the leaders of tomorrow like us to be patriotic to our country while they themselves are not patriotic.

Sixthly, we suggested that campaigning should cease because in most of the cases we see people voting for the wrong people. for example, a person comes to a place like this, most of the people are not well off. He gives them money, people won't vote for that person because they want the person to be their leader but they vote for that person because that person has provided so much to them.

Seventhly, we want equal distribution of teachers in schools. There are some schools which have so many teachers and others have less teachers and they have so many students. You may find that in a school there is only one biology teacher while in other schools there are teachers who don't they have at least a class once a week. So we were saying that we should have equal distribution of teachers in schools.

And then there is insecurity in the society: That is in the old times when you come across or when you meet a policeman you would feel you are secure, but nowadays it is not the same. You see a policeman and you feel insecure because of the things they do to the people in the society. People see a policeman, see like me when I see a policeman a just see a thief, a murderer, a rapist what they are doing to people in the society.

Then we were saying that there should be exploitation of Kenyan resources. The resources in Kenya should not be left to individuals. The government should run the exploitation of those resources and make better use of them instead of importing some things from other countries while we have not exploited ours.

And lastly the government to recognize our emergencies in that if there is an accident, the people involved first should be taken to an hospital instead of those policemen trying to tell us eti 'ngojeni kwanza mapolisi wakuje,' hapo hivyo kuna mtu amegongwa na gari and then the policemen are telling people ' ngojeni polisi wengine wakuje, they take the necessary statements as who is on fault instead of rushing the person who is there to the hospital and there are some cases like a child is drowning in a river,the child anaachiliwa hapo, nobody bothers, they bother after 24 hours or 36 hours when if it was a person from another country like tourists, immediately they get the information that a certain person has drowned in a certain river, you will see all the policemen, all the lifesavers in Kenya being hurried to go to that place to save that guy. Meaning that the Kenyans have no importance, those people from other countries have more importance than us. so we would like them to recognize our

emergencies, that's all.

Com. Asiyu: I want to ask you about the press, you have said that you want the press to tell us the other side of leaders, which is not normally portrayed when you see them on television talking. But you also know about the so called bad press, the gutter press, who create stories and sometimes will come to a leader and say that this story that you have created if you give me ten thousand shillings, we are going to publish it. This gutter press has no address, it has no physical place you can reach them, so that you can sue to be heard for justice to be done, would you still recommend in such circumstances that the gutter press be given the freedom to not only soil the names of people of Kenya but also soil the name of this country.

Awuor: In such cases, No.

Com. Kangu: Now, young girl you mentioned that our leaders are not patriotic, they invest Kenyan resources abroad. What would be your recommendation? Already we know there are those who have a lot of wealth invested out there, what should we do about it on that issue of investing outside the country?

Awuor: I guess that should be banned, investing outside our country.

Com. Kangu: And those who have already invested there can we recover that property?

Com. Asiyu: But these policemen, you see a policeman you see a thief, you see a rapist and you see a murderer, what do we do? Sack them; retrench them over all those vices, what are the recommendations?

Awuor: Not retrenching but I think the problem with them is that they are lowly paid.

Com. Asiyu: The salaries?

Awuor: Yes, that is why they behave like that. If they were paid to the recommended amount, I guess they would be doing their work well.

Com. Kangu: Thank you very much, sign our register there and Rachel Ndunge mwalimu from the same school, Kathiani Girls, Rachel Ndunge, is she there. She has gone out, she has given the memorandum. So, what about Mrs. Ndungu, she hasn't come, fine. So, let's go to Anna Wambua CBD? she has spoken. Now, Wilfred Nduso, I am sorry. Oh Winfred, I am sorry.

Winfred: Kwa majina ni Winfred Nduso CBD agent. Mimi sina la kuongeza ila yale yamesemwa na chama. Asante.

Com. Kangu: And the group of maendeleo, kama ninaita wewe na hauna la kuongeza, useme tu ukikaa mahali uko halafu we go to the next person. Tupate John Wambua senior clerical officer, John Wambua. Yuko ama hapana? Hayuko. Tupate Joseph Nduva a youth.

Joseph: Kwa jina naitwa Joseph Nduva. Yangu nimeandika na nitayasoma Waendeleo kuwa chini ya usimamizi wa Serikali kuu na kueleza vilivyo. Pasiwe na madiwani wateule popote pale. Ni hayo tu.

Com. Kangu: Thank you. Weka sahihi pale. Na bwana Ngalama.

Mulwa: My name is Charles Mulwa Ngalama. I am the chairman na wale wengine tumeandamana nao, yangu nitachangia kidogo tu.

First is the county council, second is education, third salaries of the civil servants, fourth, relieving food, fifth health, sixth retrenchment.

Upande wa county council - The revenue collected per location should be returned to the specific areas because we don't understand what revenue vile wanatumia. Now, if the top itapewa watarudisha kwa location, chief and Councillor should be there because the chief is the chairman of the locational development.

Education - The issue of education should be free from standard one to university because many people who are genius are losing education because of lack of money.

Salaries: civil servants for example those who are in low groups, they are suffering very much because they don't have enough salary and when we come to the sickness, haijui huyu ako na pesa ama hana pesa. The same thing medical allowances should be equal to every civil servant.

Relief food - instead of being given food, I suggest to be provided with water only. If it is boreholes, dams instead of relief food. We suggest to be funded money for dams or boreholes and the creation of gabions along the rivers.

Health - hospitals should be free for treatment. Retrenchment should be looked into very much because many of the people who had stretched their.. Retrenchment is causing a lot of poverty and the crime rate and yet the government is fighting for supporting ...reducing poverty in a way that they are using money to see that they are eradicating poverty. Retrenchment is causing more poverty, crime rate and yet the government is using a lot of money to fight the same, so we don't support retrenchment.

Com. Kangu: Is that all?

Mulwa: Yes.

Com. Kangu: Thank you, anything? Asante na uweke sahihi pale. Tupate Michael Nzau, hayuko? Basi tupate Grace M. Mulwa businesslady.

Grace: Kwa majina naitwa Grace Mulwa, I am a businesslady.

Com. Kangu: Chukua hiyo microphone na usishike hapo mwisho kwa sababu hapo ndio..

Grace: Langu la kusema ni ile imeongezwa na ma-chairlady wetu, nitaongeza kidogo. sasa sisi wanawake tuko na shida nyingi sana kwa vile umesikia tuko na shida ya aina hii. Vile umesikia watu wanataka kufanya kazi kama mama, na anazuiwa kwenda kufanya hiyo kazi. Sasa tutafanya nini ndio nyinyi mtusaidie ndio umaskini usiwe. Kwa sababu najisaidia sana na kusomesha mtoto na akifika form four hawezi kupata kazi. Nimeuza kale kashamba kangu na hakuna kazi amepata.

Siku hizi ndio unasikia watu wakisema masomo haina maana kwa sababu sina mtu wa kunisaidia ili mtoto wangu apate kazi. Nikiwa niko na mtu wa kunisaidia anaweza pata kazi. Lakini kama sina mtu hatapata kazi. kingine ni vile umesikia hiyo ni risk allowance. Wale wanafanya kazi kuna wengine wanasema habari ya risk na huyo mtu anaenda kufanya kazi pahali pabaya na huyo mtu anashika shika uchafu sana na risk allowance inaletewa wengine na wengine hawapati na kila mtu anashika shika uchafu.

Ikiwa ni kama hawa watu wa maofisini, anapata risk allowance lakini kuna mtu yule anashikashika uchafu sana huko tuseme kama kwa ma-wards na hapati risk allowance. Kwa hivyo kama munaweza kutusaidia munaweza kusaidia hawa watu wako na hiyo shida kwa sababu ile ingine mmeongezewa hiyo salary inakuwa ni nyingi mtu anafanya kazi nyingi sana. Inasemekana mtu vile amesoma ndio anapata lakini kazi ile mtu anafanya akiwa chini anafanya kazi mingi sana. ni hayo tu mtusaidie Katiba kwa kutuungalilie watoto wetu wakisoma wapate kazi wale hawana kitu cha kujisaidia. Asanteni.

Com. Kangu: Asante, na tupate, Mary M. Nthiani.

Mary: Chairman na makamishina wote na wale walioko hapa kwa mkutano huu. Yangu ni kusema, jina ni Mary Nduku Nthiani. Ninazungumzia mambo ya nyumbani, mambo ya nyumbani namna gani? Sisi wanawake tumepata shida sana. Wanawake wamekuwa watu wasio na maana kwa wanaume, kwa maana wanawake wameuawa kinyama, kila siku na hatujui ni kitu gani kinawafanya wanaume waue wanawake na wanawake ni dawa ya wanaume, na sijui ni kwa nini mwanamke auawe na mwanamume. Na kama mwanamke hayuko kwa nyumba, hiyo nyumba haina raha. Watoto wanauawa kila wakati na kazi

nyingi za nyumbani wanawake ndio wanafanya na wanawake ndio wanatafuta pesa na wanaongoza watoto na wanaongoza hata wanyama walioko nyumbani na mwanamume akija anaanza kumpiga yule bibi, na yeye mwanamume ameondoka asubuhi na mapema kama saa kumi na mbili hata wengine hawajulikani na watoto wao.

Com. Ayonga: Kwa hivyo toa maoni.

Mary: Nasema wanawake wapatiwe haki yao na waache kupigwa, na waache kuuawa. Kwa hivyo makamishina waangalie hilo neno.

Kingine, sisi wanawake mabwana wetu wanaenda kufanya kazi na sasa kuna retire ya wanaume na wafanyikazi hata wanawake na hiyo retire ikifika mtu akimaliza kazi yake anaambiwa aende nyumbani na akipata hii barua ya kuenda nyumbani hana pesa, sasa huyu mtu akija nyumbani na hana pesa amekuwa kama yule ambaye hakufanya kazi kwa hivyo ninasema kamishina mtu akipatiwa retire apatiwe hata pesa zake aende nazo nyumbani mara moja.

Kingine tuna wanawake wanaofanya kazi na hiyo wanawake wakifanya kazi na wengine wanazaa wanaenda maternity wapatiwe muda wa kupumzika ili yule mwanamke apate nguvu ya kuenda kazini na atengeneze mtoto wake na huyo mtoto awe na nguvu. Kwa maana wanaume hawajui kuzaa kama ni kitu kigumu sana, lakini wanawake wanazaa na wanasikia mwili hauna nguvu lakini wanapatiwa siku kidogo sana za kurudi kazini. Kwa hivyo ninasema wanawake wapatiwe nafasi nzuri, akipatiwa maternity leave. Apatiwe nafasi nzuri ya kupata nguvu, akunywe ile supu na atengeneze mtoto wake. Ndio tunakunywa supu ndio tunapata nguvu ya kuenda kazi.

Kwa hivyo kuna ingine mwanamke kama mimi, bwana yangu akifa wale wandugu wa yule bwana wanakuja kunyakua ile mali yangu na mimi ndio nilikuwa bibi wa huyo bwana na akifa ile mali yangu inanyakuliwa na ndugu zake na ninaambiwa niondoke. Sasa nitaenda wapi na kwetu hakuna nyumba? Mahali nilitoka kwa baba yangu nilikata hiyo kauli na sina mali huko kwa baba yangu. Sasa hiyo Commissioners muangalie. Mwanamke, bwanake akifa ile mali iko ya bwana ilikuwa ni ya bwana na bibi, na watoto wake. Kwa hivyo muangalie hapo.

Upande wa hospitali - hospitali sisi tuko na taabu sana, mwanamke akizaa anatakikana pesa hata akiwa mgonjwa anaititshwa pesa na hizi pesa hakuna kwa hivyo dawa zikiwa za bure ni vizuri. Hospitali iwe ya bure kwa maana wengine ni maskini na wengine wanakufa shauri ya kukosa pesa. Mtu akipelekwa huko kwa kupasuliwa ni elfu moja, kwingine ni elfu mbili na wengine hawajui noti ya elfu ni gani, hata hawajui inaandikwa namna gani. Pesa ya elfu ni kubwa sana kama wakati wa leo na sisi hatufanyi kazi tunakaa nyumbani. Kwa hivyo matibabu yawe ya bure.

Upande wa elimu - elimu kama ikiwezekana kutoka nursery mpaka university iwe ya bure.

Kuna kitu kingine, ile tunachagua ma-MP na tunachagua ma-Councillor, hiyo ni hali moja. MP kama tunamchagua na hatusikii akizungumza habari ya kwetu mahali alichaguliwa kama bado kumaliza mwaka tumtoe, aondoke kabisa aturudie tumchague mwingine kwa maana tukimchagua amalize miaka tano na anajua hakuna ingine anaenda anakaa na anatusahau, hata hajui sisi ni akina nani. Anaenda kabisa na anangojea ile miaka tano tena aje atuitishe kura. Hiyo tumekataa. Kama ni mwaka mmoja tuangalie anatufanyia nini tuseme huyu mtu atoke, tumchague mwingine, hata Councillor namna hiyo. Kwa hivyo tunaona kitu cha namna hiyo ni kibaya sana kwa mtu tunayemchagua na anakaa miaka tano na anajua nitamaliza ile miaka mitano tena niende niwaitishe kura. Sasa tumeamka na tumejua hali ya dunia iko namna gani, kwa hivyo makamishina mujue tumeamka. Na wale tunawachagua wajue tumeamka.

Na kuna ingine, ile kiwango ya lugha kama Kenyaiwe na lugha mbili Kiingereza na Kiswahili.

Ile ingine, ni ukabila. Sisi hatutaki ukabila, kama mkenyahata akitoka hapa aende akae Busia ni mkenya, hata akitoka hapa aende Marsabit ni mkenyana tunataka kila mkenyaawe na uhuru ya kukaa kila mahali anataka. Kama sisi tuko hapa Kathiani, mtu akitoka Marsabit anakaa hapa Kathiani, tunajua yeye yuko kwao. Kwa hivyo sisi hatutaki ukabila.

Upande mwingine tunataka kama title deed zinatoka kama mimi bwana yangu amekufa nipatiwe title deed ya ile mali yangu kwa maana mimi ndio nilikuwa bibi wa yule mtu. Nipatiwe title ya mali ya bwanangu. Kwa hivyo kitu kingine ni unywaji wa pombe. Unywaji wa pombe sisi hatutaki, wamama wamepata taabu sana kwa unywaji wa pombe. Wanaume wamekuwa hata hawana nguvu ya wanawake kwa shauri ya pombe na hii pombe imetiwa madawa mingi sana inaharibu watoto wetu, inaharibu mabwana wetu na hiyo pombe sisi hatutaki, ile pombe inaharibu watoto wetu na hiyo pombe inaharibu watoto wetu sisi hatutaki.

Kuna kitu kingine, tuna ma-chief na assistant chief na zamani walikuwa wanafanya mambo mengi ya kusaidia DC na hayo mambo sijui yametupiliwa mbali kwa hivyo ningesema makamishina hayo mambo, hiyo kazi ilikuwa ya assistant chief na chief wafanye ili DC awe na kazi nyepesi kwa maana kazi yote ikiwa ya DC, sisi tutakuwa hatuna huruma nzuri. Kwa hivyo ningesema yale mambo yalikuwa ya zamani ya akina chief, assistant chief watufanyie, ili DC awe na mambo kidogo. kwa maana ninaonelea DC saa ingine anakuwa na mambo mengi na tunapata huduma isiyo nzuri.

Kwa hivyo kitu kingine ni tamaduni wetu. Kila kabila iko na utamaduni zao. Kama sisi Wakamba tunajua kitu kinaitwa 'kithitu' ndio inafanya sisi tusinyang'anye watu wengine mali yao, kwa hivyo hicho kithitu tunataka kiwe namna hiyo vile kilikuwa zamani. Kithitu kiwe upande wa Ukambani kwa maana sisi ni Wakamba na tunajua nikikupatia kithitu huwezi kuninyang'anya mali yangu. Kithitu iwe! Kama kamishina hujui kithitu uniulize ni nini.

Com. Kangu: Ninaelewa kithitu kabisa mama.

Mary: Kwa hivyo kila mtu ana utamaduni wake. Na kila tamaduni sisi kama Wakamba kama bibi anaolewa na hakuna zile mbuzi tatu za kuoa bibi hiyo ndio harusi ya mkamba. Kama mtu hapeleki hizo mbuzi kwa baba ya msichana, hana bibi, hiyo mbuzi iwe mahali pale kwa maana hiyo ndio harusi ya mkamba na kama hakuna hiyo mbuzi bibi hakuna.

Kuna kitu kingine, mwanamume anaoa bibi na huyo bibi mwanamume akiona ako na gharama kubwa anamtupilia mbali. Anazaa watoto watano, wasita na anamtupilia mbali kwa maana anaona mambo ni magumu na anaona uchumi ni mgumu, na bibi anaenda na watoto wake, na huyo bibi anaenda anakaa anapata kibarua anatumza hao watoto wake na watoto wanakuwa na huyo bibi bado kuolewa na mtu mwingine, yeye anakaa anatumza watoto wake. Hawa watoto wakiwa wakubwa wanataka kurudi kwa baba yao, kwa maana watoto hawajui shida iliyokuweco ya mama na baba, watoto wanataka kurudi kwa baba yao, watoto wajengewe na huyu bwana kwa maana yeye ndio aliwazaa hawa watoto na mahali nilitoka kwa huyu bwana sikupata mtoto mwingine. Nilienda na hawa watoto na nikakaa na nikapata shida na hawa watoto na nikawalea, wakiwa wakubwa warudi kwa baba yao, na wakirudi huyu baba awakatie hawa watoto shamba yao wajenge. Kwa maana nikienda kwa huyu bwana sikuwa na watoto, ndiye alinipatia watoto na kama ningekuwa peke yangu siwezi kupata mtoto lakini nikiwa na bwana ninapata mtoto. Na huyu mtoto ni wa huyu bwana.

Com. Kangu: Jaribu kumaliza mama ingawaje maneno yako ni mazuri.

Mary: Kitu ingine sisi tuna wasichana na msichana leo hataki kuolewa. Msichana akikaa kwa baba yake agawiwe shamba pamoja na yule kijana, huyu msichana ni mtoto kama yule kijana na akikataa kuolewa kwa maana siwezi kuweka msichana kamba nimuuzae akae kwa baba yake na apatiwe shamba pamoja na kijana. Lakini yule aliolewa akae kwa bwana yake, kwa hivyo maneno yangu yanakoma hapo.

Com. Asiyu: Mama Umeongea juu ya uchovu wa wanawake wakipata watoto, unataka wapewe nafasi nzuri ya kupumzika kabla ya hawajarudi kazini, yaani maternity leave lakini hajapendekeza ni muda gani.

Mary: Wapewe miezi mitatu.

Com. Asiyu: Na hii kithitu, unaona hapa Ukambani iendelee namna hiyo. Na kuna makabila mengine wana kitu kama hicho cha kithitu tena kama wajaluo wana muuma, wengine wana ingine. Ungependelea hata makabila wengine waendelee na hiyo tabia yao ya zamani?

Mary: Si kila kabila wako na utamaduni wao na sijui wajaluo wanapendekeza nini. Sasa kama wako hapa tukajadiliana ndio vizuri. sasa nitatoa wapi wajaluo na kama wako hapa, tutajadiliana.

Com. Asiyu: Shida yangu ni kwa vile ulisema ya kwamba kuwe na lugha mbili tu. Kiswahili na Kiingereza. Sasa kama hakuna

lugha hata hizi tabia hakuna. Tuendeleo na kuongea lugha yetu au tuseme hii lugha mbili peke yake, tuache lugha zetu.

Mary: Hapana lugha zetu ziko na hiyo ndio lugha ya mama. Tunataka ile ingine ya kutembelea nchi zingine. Hiyo ndio kitu nilikuwa nasema. Kamishina kuna kitu nimesahau, naweza kusema?

Com. Kangu: Sema hiyo umesahau.

Mary: nimesahau upande wa shule. Sisi kama wazazi, tumesikia ile adhabu ya kiboko imeondolewa na, hata sisi watoto wetu nyumbani tunashika kiboko na wengine watoto wetu hata wengine ni wakubwa kushinda waalimu. Na hawa waalimu watoto wetu wameona waalimu ni kitu kidogo sana, hata wanapuza hawa waalimu kwa maana kiboko imeondolewa. Kama ingewezekana, ningesema kiboko ndio kinatunza mtoto hata nyumbani. Kiboko ndio kinatunza mtoto hata nyumbani sisi tunashika kiboko. Kwa hivyo Ningependekeza waalimu wasiumize watoto lakini kiboko kirudishwe.

Com. Asiyu: Wachape hawa?

Mary: Wachape hawa kwa maana waalimu ni wazazi na kama hii kiboko kimewekwa chini, hata watoto wetu wataharibika na watoto watapiga waalimu.

Com. Kangu: Sawa asante sana. mama asante sana andikisha pale, umesema maneno mazuri tunaelewa mambo ya kithitu, hata mimi najua clan huku Ukambani mbai wakichukua hatua, hakuna mtu anacheza. So, mama amesema pengine kwa administration of justice turuhusu mambo ya kinyumbani isaidie na pengine itasaidia kwa shida nyingi. Tumsikize sasa Francis Kimondio. Amezungumza kwa niaba yako, asante sana basi bwana Francis. Tupate bwana Boori. Okey, tupate Peter Muli, chief, amezungumza fine na Samuel Mumo, PTA chairman. Imesemwa na Mary tayari. James Ngisiu, ni Ngisiu ama ni Nguyo? James Nguyo, endelea.

Nguyo: Nashukuru chairman wa Commission hii, makamishina na wote walio hapa. maoni yangu ni kama ...

Com. Ayonga: Majina kwanza

Nguyo: Majina yangu ni James Nguyo. Maoni yangu kwa kweli yametolewa na wengi lakini kuna moja tu ningetaka niongezee. Ningependa nitoe maoni kuhusu utawala. Unajua utawala ni laini ndefu sana inanzia huko chini kwa mzee wa kijiji, assistant chief, D.O na kwenda juu na wote najua ni maafisa. Najua kwa hakika kila ofisaa ana kazi yake ambayo huwa anatekeleza na naenda tu kutoa maoni kuhusu yule ofisaa wa chini sana mzee wa kijiji. Huyu mzee kama afisaa huwa anafanya kazi kwa njia tu ya kujitolea (voluntarily). Na ni maoni yangu kwamba hii Commission naiuliza kwa maoni huyo kama ofisaa apewe mshahara, awe akilipwa ndio apate kutekeleza kazi yake vizuri. Hayo ndio yalikuwa maoni yangu. Asante sana.

Com. Kangu: Na swali moja, kwa wakati huu hao wazee wengi, wanachaguliwa na ma-chief na assistant chiefs wakiwekwa kwa mshahara sasa tuwe na proper employment procedures ama waendeleo kuwa watu ambao wamechaguliwa na chiefs.

Nguyo: Kuwe na proper... njia ya employment.

Com. Kangu: Weka sahihi. Nafikiria kwa sasa tumpatie mheshimiwa nafasi na yeye aweze kunena yale ako nayo.

Hon. Kaindi: Asante sana. Kwanza ningetaka kuchukua nafasi hii kwa niaba ya watu wote wa Kathiani, raia na wananchi kuwakaribisha nyinyi Commissioners mkiongozwa na daktari Mutakha Kangu, ma-Commissioners ambao wamefika hapa Phoebe Asiyo, com. Charles Maranga na Pastor Ayonga. Shukrani kwa kufika, nadhani mmeona watu wetu wako tayari kutoa maoni yao kuhusu sehemu hii muhimu zaidi ya nchi yetu. Sisi tukiwa watoto wadogo hapo zamani tulikuwa tunaona viongozi kama akina Martin Shikuku na wengine wakijivunia vile walitoka nchi ya Kenyawakaenda kule uingereza Lancaster House kuandika Katiba. Mimi naitwa mheshimiwa Kyalo Kaindi, mbungewa Kathiani.

Tukiangalia safari iliyopigwa na viongozi wetu wazalendo miaka ya sitini, kutoka nchi ya Kenyawaende mpaka Lancaster House uingereza wakaandike Katiba, hata mpaka wa leo ni jambo la historia. Na sisi ikiwa wananchi wa Kenyawenyewe tumepewa nafasi ya kuandika Katiba yetu, hii ndio the first issue ya human rights. Hakuwezi kuwa jambo lingine muhimu kuliko hili. Hata wakati mwingine nilikuwa nafikiria ukumbi kama huu utakuwa umejaa kwa sababu ni wakati wa historia kuandika upya Katiba yetu. Ningetaka kusema sheria ambazo sisi kama Bunge hutumia zinatokana na Katiba.

Katiba ambayo iliandikwa wakati ule na Katiba ambayo imekuwa ikirekebishwa muda kwa muda wakati kwa wakati na Bunge letu. Kwa hivyo wakati mnaandika Katiba leo mjue mnatuandikia zile sheria ambazo tutakuwa tukizitumia katika Bunge. Kwa hivyo umuhimu wa maoni yenu, umuhimu wa yale maoni ambayo mnatoa leo ni umuhimu wa juu zaidi. Yale utayaeleza leo hapa, unatengeneza sheria ambazo mbungewako atatumia, ambayo nchi yako itatumia, ambayo President wako atatumia kwa vizazi vijavyo kwa miaka mingi sana. Kwa hivyo ukitoa maoni na nimesikia vile mnayatoa ni maoni ya muhimu sana. Nilikuwa nataka kuyasema yale ili niweze kusema machache pia.

Ninajua leo na kesho tunafanya hapa, kesho tutakuwa sehemu ya Athi River, nimepitia asubuhi niangalie vile wanavyojitayarisha na huko ni wengi na mtawakuta wengi sana, wako tayari pia kutoa maoni kama hapa. Ningetaka kuguzia kidogo mambo mawili matatu kwa sababu nimesikia wananchi wetu hapa wamejaribu kuyaeleza yale yao na yale wanayaeleza ni mambo ambayo yatajenga nchi yetu.

Jambo moja ambayo kabisa nimesikia wakizungumza ni ile protection ama vile tunaweza kusaidia watoto wetu ambao ni minors na mama mmoja ameongea sana, kusema shida ambayo wanapata, shida kubwa tuta-protect wale watoto wadogo kwa njia gani, na wanapendekeza kuwe na njia ya ku-protect ama ya kusaidia wale ijapokuwa hawasemi ni kwa njia gani, wanasema

Katika sheria yetu tuwe na sehemu ambayo inaweza kusema wewe ukiadhibu mtoto ama ukiumiza mtoto lazima uchukuliwe hatua hii. Nimesikia wakisema yale na ni mambo ambayo ni lazima na sisi pia tuhaikikishe yamesemekana vile yalivyo.

Sehemu ya watoto wameongea juu ya watoto ambao wanazaliwa nje ya ndo na nimesikia wakiongea na wakitoa maoni yao kusema watoto hawa ambao wewe unazaa mtoto na unatoroka, unaacha pengine mama ama na mama pia anatoroka, anaachia mzigo mama mzazi, wanasema tuwe na sheria na tuwe na kifungo kimoja Katika sheria ambacho kinaweza kusaidia na kuhakikisha wewe ambaye umetoroka na umezaa una jukumu la kuangalia kwamba yule mtoto amelindwa na amelelewa vilivyo. Wanasema kwa hivyo sheria za watoto ijapokuwa tumekuwa tukipitisha bungeni, wanazingatia ziwe ni sheria ambazo zinaweza kuangalia tukizaa mtoto, you are responsible kuangalia maneno ya yule mtoto.

Nimesikia kidogo wakiongea juu ya uhuru wa magazeti na nimefurahi kwa sababu wamekuwa very clear. Tuko na mtoto mmoja msichana amesema waandishi wa magazeti wapewe uhuru wao waweze kuandika na hiyo ni sawasawa, lakini nimesikia Commissioner akiuliza, je, na wale wanaandika maneno ambayo ni ya uchafu, maneno ambayo hayajathibitishwa wafanye nini? Mimi nataka kusema katika Kenyayetu ni lazima tutofautishe juu ya gutter press na magazeti na vyombo vya habari ambavyo vinatoa habari ambayo ni ya kweli, ukitaka kujua wamekuwa licenced unaweza kwenda K.B.C, ukitaka kwenda kwa standard unajua standard wako kwa ofisi fulani, ukitaka kwenda kwa nation wako ofisi fulani, kwa hivyo hata ukitaka kuwapeleka kotini kwa matamshi yao, kwa maandishi yao, unajua utawapata wapi.

Juzi, labda hamjui katika Bunge letu, tumeona hata mawaziri wamefungwa minyororo, wanaambiwa bibi yako alizaa na mhindi, wanaambiwa fulani alifanya hivi, yaani ni maneno machafu ya kuharibia watu sifa kwa sababu yule waziri hawezi kusimama na kiongozi, hawezi kusimama na kukanusha kusema sasa bibi yangu hakuzaa mhindi. Ataleta bibi yake asimamisha mbele ya nchini ya Kenya yote, aonekane hakuzaa na mhindi kweli? Kwa hivyo tunasema tuwe na sehemu mbili za uandikishaji. Tuwe na magazeti ambayo yanatambulika na yakiandika yaandike maneno ambayo ni ya kweli. Na magazeti yaache kuandika maneno ya siasa peke yake. Yaandike maneno ambayo yanasemwa hapa maneno ya raia, maneno ya maendeleo ya nchi yetu. Hapana maneno ya siasa siku zote. Ukifungua nation leo ni maneno ya siasa, ukifungua standard ni maneno ya siasa, ukifungua people ni maneno ya siasa, lakini maneno ambayo yanahusu raia wetu hapa yanapewa huku ndani kidogo kidogo ndio yanapewa sehemu kidogo. tunataka maneno ya maendeleo ya nchi yetu, mipangilio ya nchi yetu katika vyombo vya kama radio yapewe umuhimu zaidi na haya ndio yale mambo nimesikia kidogo yakitoka kwenu. Amesema kitu kimoja ambacho ni cha maana sana, tuwe na uzalendo wananchi wa kenya. Uzalendo ni kusema nini? Mali yako ikiwa wewe umepata mali, kwa nini unataka mali uende upeleke uingereza. Unataka kupeleka South Africa ya kufanya nini? Kwa nini hutaki ile mali pia ifaidi wananchi wetu. Ikiwa umepeleka benki zetu hapa, ikiwa ni standard bank, wananchi wetu wataweza kujipatia huduma ya loans, wanaweza kufaidika na zile pesa zako. Lakini ukipeleka nje wananchi wamesema very clearly hiyo ni makosa. Wangependelea sehemu ile kubwa ibaki hapa nchini kwetu. Na mimi nina hakika wanasema jambo moja. Hakuna ubaya mwananchi wa Kenya kwenda kufanya kazi nchi ingine, na hakuna ubaya hata mwananchi wa Kenya kuanzisha viwanda na kutafuta mali sehemu zingine kwa sababu wananchi wetu wa Kenya wameenda sehemu nyingi kufanya hiyo. Lakini tuwe na sehemu moja kidogo ambayo wakipata

mapato kule inaweza kurudi hapa nchini na kufaidi wananchi wetu.

Maneno ya upigaji wa kura, tunakubaliana na hawa 100%, pesa zikome wananchi waweze kuchagua viongozi, sio kupitia kwa pesa wachague viongozi kwa sababu kiongozi anafaa na anaweza, na yale ndio wanasema wazi lakini ni rahisi kusema yale lakini Rais akipitia Kathiani wanataka pesa. Labda tuko na nusu ya sehemu ya hawa ambao watataka kuningojea pale nje wanione tukimaliza hiki kikao. Waniambie mheshimiwa maneno ya busfare iko namna gani? Mheshimiwa hata lunch sijakula na yale mtayaandika wapi kwa katiba. Si ni nyinyi, tutaandika wapi sehemu hiyo? Kwa sababu tukitoka tutakuwa na mkutano mkubwa, labda wengine watatoka kule kuangalia kama mheshimiwa sasa anaweza kuwa anabeba kitu.

Ikiwa tutaweza kusaidia watu wetu, walikuwa wametengeneza civic education, masomo ili watu wetu waweze kuelewa haki zao vile wanaweza kujimudu, kujimiliki na kuendesha mambo yao. Civic education iwe continuous. Hapana, kwa sababu tunaandika katiba inapewa na inaenda. Makanisa yetu yamekuwa yakiendelea kuandika kwa nini hawajapewa nguvu za kuendelea kuandikisha, kuendelea kupeana hiyo elimu katika sehemu za makanisa? Kwa nini pesa zimepewa vikundi fulani wakati huu wa katiba. Ninajua ni kwa nini kwa sababu tunataka kuelimisha watu wetu, lakini kwa sababu tumeonelea ni jambo la kufaa, tunauliza wananchi wetu wawe wakipewa yale. Ikiwa ni kupitia kwa makanisa ama vikundi vya akina mama hawa, hawa wamama wana sehemu kubwa zaidi kama hapa kwetu Kathiani.

Kila sub-location iko na vikundi hazihesabiki za akina mama. Wako na utaratibu wao, utakuta tuko na chairlady, tuko na nani wanafuatana mpaka chini. Kwa hivyo ikiwa tunapendekeza civic education, kwa nini tusikuwe na wamama ambao wameelimishwa katika vile vikundi, wawe wanaweza kuelimisha wale wengine wakati wamekutanika kule kwa mikutano yao. Kwa nini tusitafute vikundi kutoka Nairobi, kutoka kwingine ambao ni professionals kwa nini? Ile lugha ya wamama, ile hawa wamama wanaelewa wao wenyewe na mimi nina hakika baina ya wale wamama na ile lugha yao wanaweza kupeana elimu ya kutosha na ya kufaa zaidi ambao wataielewa wao wenyewe.

Mwingine amezungumza juu ya kazi ya polisi, role ya polisi na msichana amesema, ako na shida sana. mimi nikitoka Nairobi, Athi River kupitia sehemu hiyo, nimekuta vituo kama nne, traffic police. One kilometer traffic police anasimamisha gari, another kilometer traffic police anasimamisha magari, hata hawana aibu ile kitu wanataka ni pesa na unaona wakichukua tu, ni pesa, ni pesa. Ni sheria gani ambayo tumekosea? Sasa polisi wamekuwa ni idara ingine ya kuokota kodi, kodi ambayo haitufikii sisi wenyewe ijapokuwa matumbo yao na watoto wao. Ni lazima tuwe na sheria ambazo zinaongea katika nchi yetu. Mheshimiwa anaona polisi anaungana na hana njia ya kumwambia 'ee officer simamisha hiyo' our laws must speak. Sheria zetu ziweze kuongea. Kusikuwe kuko na sheria ya polisi. Polisi si sheria ya raia, sote ni wananchi wa kenya, na ikiwa yule anafanya makosa, tuwe na njia ya kushika yule na kuhakikisha makosa hayafanyiki tukiyaona wazi.

Taabu ya sheria zetu ambazo tuko nazo leo, ni kwa sababu sheria moja inasema wewe ukipatikana unaiba kuku, miaka kumi na viboko. Mwingine akichukua milioni moja, anafungwa miezi mitatu ama mwaka mmoja. Tuko na shida kidogo hapo kwa sababu kwa nini sheria inaangalia yule mwananchi wa chini kabisa. Ndiyo, kuiba kuku si kitu kizuru, si ni kweli? Lakini huyu

ameiba milioni ishirini, milioni mia moja ameangamiza idaya ya serikali ambayo ingesaidia wananchi maelfu na maelfu. Yeye anapewa miezi mitatu. We must avoid discrimination and ambiguity it in our laws. Kwa nini judge aambiwe kwa mfano, unaweza kumtoa fine ya shilingi kutoka elfu moja mpaka milioni moja, kutoka elfu mbili mpaka elfu mia tano. Si ma-judge ni binadamu. Mishahara iko pale chini. Basi, ndiyo inatupatia ile nafasi ya ufisafi. Unakuta katika koti zetu kuna makarani wa kulainisha hiyo na kuwa na kangaroo courts. Judge amesema wewe hata usipojitetea, utakuwa na nini? Na shida. Hata imefika kwa ma chief wetu hawa, unakuta kangaroo courts. Raia akishikwa amebeba kuku kwa sababu yule mama amesema hawataki pombe kuna anaachiliwa na hajulikani aliachiliwa kwa njia gani. Sheria zetu ziwe specific. Tuwe na sheria ambazo hazina discrimination. Sheria ambazo ni straight forward. Ukiwa umeiba, umeiba na hukumu ni hii. Why are we subjecting our laws to interpretation mahali kwingine? Kwa sababu interpretation ndiyo inaleta shida, discrimination ndiyo inaleta shida, tuwe na sheria ambazo zinaweza kuzungumza. Raia anajua makosa ni makosa. Umeiba kuku, utafungwa hii na maneno kwisha. Siyo eti judge aangalie kama atakufunga mwaka mmoja na uliiba kama yule mwingine, yule mwingine alifungwa miezi, wewe unafungwa miaka kumi. Lazima tuwe na sheria ambazo zinaangalia watu wetu. Sheria siyo za kuangamiza nchi, sheria ni za kurekebisha nchi. Na ikiwa tunaelewa sheria si za kuangamiza ni za kurekebisha, basi tutengeneze sheria na kurekebisha. Kwa mfano ukiangalia zile sheria hata sisi tunatengeneza kule Bunge, all the time, Commissioners wa income tax kupitia kwa wizara ya finance, wanasema, fine mwaka huu kila budget, usipofanya hii, fine inakuwa kutoka elfu kumi hadi mia moja mpaka siku hizi zingine zimefika milioni moja na hatuelezwi ni wananchi wangapi ambao hawaku comply na hiyo. Why always have stiff penalties, stiff penalties. Kwa nini? Ndiyo tumesema hata makosa mengine katika nchi yetu, hakuna haja ya mtu kupelekwa kule jela. Kuja hapa utulimie barabara zetu, kuja hapa ujenge hospitali zetu ukisimamiwa. Community polising badala ya kupeleka mtu ambaye ameiba kuku, leta hapa kwetu. Wacha tukienda kwa assistant chief tukakute watu wanatufanyia barabara zetu. Kwa sababu ni wengi tutapeleka Machakos kufanya nini? Unawapeleka Langata kufanya nini? Sheria si ya kuuwa, sheria ni ya kutengeneza. Wakienda kule jela, wamejazana huko, ukimwi umejaa kule, ukienda jela siku hizi, ni afadhali hata kunyongwa. Kwa sababu huko utakufa na ukimwi. Kutoka ni ngumu sana. Kwa hivyo tunataka sheria ambazo zinasema makosa kama yale, yarekebishwe hapa kwetu na tuwe na sheria ambayo inaweza kuhakikisha kuwa wananchi wetu, tunawatumia kwa kurekebisha badala ya kumaliza na kuua.

Iko mama amesema kitu ambacho ni cha muhimu sana. Disaster, emergency. Msichana alisema sheria zetu zihakikishe umuhimu wa maisha ya watu wetu. Haupelekwi chini? Umuhimu wa maisha ya watu wa Kenya. Siku hizi ukipita unasikia, hii manhole, watoto wa shule wawili waliingia, wananchi nimeona Nairobi wakilalamika, tumejaribu kuita police, tumejaribu kuita watu wa city council, hakuna mtu anakuja kutusaidia kutoa mwili. Kwa nini sisi hatuna furaha na umuhimu wa maisha yetu. Kwa nini tunachukua maisha yetu kama mzaa, kama mchezo tu. Vyombo vyetu kupitia kwa sheria. Tuandike sheria ya mwananchi wa Kenya iwe ni sheria ya kuangalia mwananchi ya Kenya. Juzi kule ngambo, mtoto mdogo wa shule alipotea wakiwa katika trip ya shule. The whole country, G.S.U., nani, wote walitoka nje, kwenda kutafuta yule mtoto. Leo siingilii vyombo vya security, lakini majeshi yetu wanalala huko. Ni watu gani wanafanyia huduma. Hakuna vita, ni vita gani tumeenda kupigana?

Siku hizi tuko na department ya engineering katika jeshi, wangukuwa wakitusaidia kutengeneza barabara yetu as part of service kwa wananchi wetu. Kwa nini tuko na sheria ambayo G.S.U. yetu inaenda huko mbali na wananchi wanakaa sehemu ingine? nataka kuwapatia mfano wa ajabu, ukienda katika nchi ya Israel, kule Israel, na nimekaa Israel miezi sita, yule mtu anauza dukani, unakuta huyo ndiyo pilot wa mandege yao kukitokea vita, anaenda kupigana. Every year, lazima aende thirty days active service katika jeshi. Regular army yao, iko na watu wachache sana. Wakati huo ilikuwa askari, elfu mia tatu peke yake. Na wale wengine wako katika huduma zile za kawaida. Wanasaidia kujenga nchi. Sisi kama nchi tunajiwekea mzigo mkubwa. Kulipa jeshi ambayo haifanyi kazi. Tukitarajia siku moja tutaenda kwa vita, na wakati hakuna vita, tuendelee kuwalipa kama hawafanyi chochote? Wasaidiane na sisi. Siku hizi, ukienda army, wako na architects, wako na engineers, wako na tractors za kutosha ambazo wangukuwa wanasaidia nchi wetu nazo. Kwa hivyo pesa zetu ambazo tunalipa ziambatane na ile kazi ambayo inapewa.

Com. Kangu: Haya mheshimiwa jaribu kumaliza.

M.P. Kyalo Kaindi: Haya, sasa nitasema yangu machache. Kidogo tu. Ninataka kusema hivi, katika kusaidia wananchi wetu kwa sababu sisi kama wabunge tuko na shida kubwa sana. Mwananchi anafikiria kazi ya mbuga ni kujenga barabara, kazi ya mbuga ni kujenga hospitali, kazi ya mbuga ni kujenga mashule, Hapana! Ile kodi nyinyi mnatoa ndiyo inatakikana kufanya kazi hiyo, lakini itafanya na njia gani? Tunataka tuanzishe katika katiba, kitu ambacho tunaita consolidated fund katika kila constituency. Tuwe na trust fund and not consolidated. Trust fund zianzishwe katika kila constituency. Na ziwe zinagharamiwa directly kutoka consolidated funds, zile pesa zinakusanywa huko, sehemu moja, iwe inaletwa kwetu directly. Ikiwa ni D.O na division yake ya Kathiani, ikiwa anasimamia elfu kumi, hata machiefs wakati wanaketi na kamati zao za maendeleo, kutakuwa na umuhimu, kwa sababu watakuwa wanazungumzia pesa ambazo ziko. Kwa hivyo tunasema, tuwe na funds ambazo zimetengenezwa, ili maneno haya ya harambee ambayo yamewekelewa wananchi wetu na umasikini wao kazi ngumu sana, ikome. Harambee tubakize vitu kama harusi na makanisa. Lakini maneno ya shule, ziwe zinagharamiwa kutoka sehemu hiyo, ili wananchi wetu waweze kupumua na kufanya kazi yao. Si harambee, kila siku harambee, kila siku, na bado tunatoa kodi yetu.

Ile ingine wananchi wa Kenya wako na shida nayo ni kitu kinaitwa medical insurance. Ukienda nchi zingine, hata kama America, ukipewa nafasi ya kwenda huko, hata ikiwa ni mtoto wako, utaambiwa matibabu kule ngambo hayawezekani, ni gharama kubwa sana. Lazima upewe insurance. Na mimi nina propose, ninasema hivi, yule mtu hufanya kazi na kupewa mshahara kwa kampuni anaweza kulipa hiyo. Na mama yangu na wamama na wale wanakaa huko nyumbani watalipa kwa njia gani? Na suluhisho ni moja tu, sisi zote tunalipa kodi. Ukinunua unga, umelipa kodi inaitwa sales tax. Tutengeneze sheria katika bunge. Sehemu moja, hata ikiwa ni 5% ya sales tax yetu yote, igawiwe raia wa Kenya wote kama contribution yao ya medical cover. Na ukikataa kutumia yako ya mwaka huu, inapelekwa mbele ili siku ile utaweza kulazwa kwa hospitali, uwe matibabu yako yanaweza kugaramiwa. Tusipokuwa na insurance cover ya wananchi wa Kenya, tutaendelea kuumia, hata tukisema mahospitali yawe ya free, itakuwa ni kazi ya bure. Tupatie watu wetu capacity ya kufanya hayo mambo.

Ya mwisho ambayo ninataka kuongea juu yake ni, land tenure: Maneno ya umilikiaji wa ardhi. Sehemu hii yetu, kutoka mitamboni Kathiani, sehemu hii yote nikiwa mtoto mdogo, 1975, wali-declare areas hizo kutoka 1971, adjudication areas. Mpaka wa leo, hakuna title deeds, kwa nini? Makaratasi kule Ruaraka hayapatikani, headquarter haijatoa pesa za kutosha. Lazima tu-decentralise milikiaji wa ardhi. Kusikiliza yale makesi yako hapa kwetu, iwe katika district, ili hii kazi iwe rahisi kwa sababu ukienda kwa district leo, watakuambia tunangojea headquarter. Na headquarters inakuambia Ruaraka's technical area bado haijatoa na wananchi wanaendelea kuteseka, kuumia, hawana title deed mwaka nenda mwaka rudi. Mimi niko na mambo mengi na ninajua siwezi kuyasema yote. Nilikuwa ninataka kuwapatia tu nafasi mtoe maoni yenu mukijua mutakumbukwa katika historia ya nchi ya Kenya. Wakati unaandikisha pale, utakuwa kama Martin Shikuku, Lancaster House.

Tuliandika katiba ya Kenya. Je, wewe uliandika maoni gani ama ulikaa nyumbani kilimia kahawa yako? Na haujui kahawa itakufaida kwa njia gani bila kuandika sheria nzuri? Kwa hivyo muandike vile munaona mukifanya, mimi ninataka kusema hawa Commissioners wapewe nafasi ya kutosha, wamalize kazi yao, ama munasema namna gani?

Audience: Ndio.

Hon. Kaindi: Kwa sababu sasa tunasikia watakatwa. Hata leo, katika Bunge huko, iko mazungumzo kali, tutawaongeza miezi miwili, miezi mitatu, kwa nini tunafanya mambo ambayo siyo ya kweli. Bunge ya Kenya sisi ndiyo tulikosea hawa, for three years tulikuwa tunazozana, safari ya kwanza, tukaenda Bomas of Kenya, tutaandika katiba namna gani, na wakati Mungu amekusaidia, hata kupitia vyombo vya makanisa, wakaingilia ndani kule Ufungamano, Wakati sisi zote tumesema mungu ametusaidia tumepata Commissioners, wacha wachukue maoni na tuandike Katiba, tena zile siasa zetu na ugonjwa wetu, tunaanza kusema tena hata miezi nane zaidi, waende nyumbani wengine wanataka pesa. Nani anataka pesa katika hawa? I know them, Phoebe Asiyo alikuwa mbunge kama mimi nikiwa shule. Maranga amekuwa ... nani hajui hawa? Tunaanza kusema wanataka wajiongezee pesa. Pesa gani? Tunakubaliana katiba ni muhimu ama si muhimu?

Crowd: Ni muhimu!

M.P. Kyalo Kaindi: Na kwa nini tusiwapatie nafasi ya kuandika katiba. Mimi nasema tuwapatie.

Lakini la mwisho ya Kathiani ni moja, katika zile sheria za kutengeneza boundary ama mipaka ya sehemu ambazo tunawakilisha katika bunge, mimi constituency yangu inatoka Nairobi, kule Embakasi, ninagawanya na Mwenje. Ninaenda umasaini ninagawanya na Prof. Saitoti, ninaenda sehemu ya kule Kasarani ninagawanya na Muchiri. Inapitia sehemu hii yote ndiyo hiyo inapita hapa tuko ni kama tuko katikati, inaenda mpaka milimani ya Mbooni. Hiyo ni constituency ya aina gani? Mheshimiwa kwani ni mvua? Anaweza kuwa sehemu hizo zote wakati moja na njia gani? Tunasema wakati tunatengeneza katiba, hata sehemu za Electoral Commission, zitengenezwe, tuwe na nafasi ambayo tunaweza ku-review boundaries zetu za sehemu za uakilishi ili tuwe na constituency ya Kathiani vile wananchi wanataka, constituency ya mji kama Athi River vile wanataka, ili huduma ikuwe rahisi. Otherwise tutaendelea kusema, Kaindi alikuja hapa kwetu mwaka mwingine. Na ukipitia hapa, raia milioni na milioni wanataka huduma. We are 93,000 people sehemu ya Kathiani division. Athi River division, 67,000 people

look at all that, na wabungewengine wanawakilisha watu elfu tatu, enda kule Marsabit, waziri mmoja anawakilisha elfu tatu, registered voters. Sasa ikiwa anawawakilisha elfu tatu na mimi ninawakilisha, sasa tumeandikisha 67,000 people, na ni kwa sababu watu hawakuelezwa, Athi River yenyewe inaweza hata kuandikisha hata 50,000 people peke yake. Tutahudumia wananchi wetu kwa njia gani ikiwa mambo yako namna hiyo? Kwa hivyo katika mipaka tukumbuke wakati huu tunaandika katiba, sehemu iwekwe ya kusema mipaka pia ibadilishwe. Asanteni sana.

Com. Kangu: Basi, asante mheshimiwa kwa maneno umenena mazuri. Na mimi nataka kuongeza kwamba, if Kenyans squander this opportunity, mtalia. It is a very rare opportunity we have, kama wa Kenyasisi wenyewe kujadili na kuzungumzia mambo tuamue tunataka kuendesha maneno kwa njia fulani. Na ni maneno yataendesha maisha yenu kwa mda mrefu. Saa zingine hata siyo ninyi wenyewe. Ni watoto wenu. Lakini kuna wengine wanataka kuendesha sasa kama tulianzisha tu maneno ya kuangalia kura hii yenye inakuja saa hii. Ukikubali yaende hivyo, mtalia. We must not squander this opportunity. Imechukua wa Kenya 10 years to fight to get this opportunity. Ikipita saa hii tumetengeneza katiba mbaya, baada ya miaka mitano muanze kusema tena katiba mbaya? Kuna wale wataambia ninyi, si mmetengeneza katiba juzi tena munataka kutengeneza namna gani? Hamjui itawachukua mda wa kiasi gani tena kupigana na kusema itengenezwe. So let us not squander the opportunity.

Nataka tuendele mpaka saa saba na nusu, halafu tutachukua break ya about 35 minutes ndiyo tena turudi, tuweze kuendelea. Sasa tumsikize Raphael M. Makau ama assistant chief hautaki kuzungumza? Basi sawasawa kama umezungumza, Joel Munyao, business mana. Hayuko. Reverend Gideon Mbithi, tumsikilize basi bwana reverend.

Rev. Gideon Mbithi: Basi, asante sana mwenye kiti na Commissioners wale wengine pamoja na honourable M.P. na wananchi wote. Ningetaka kuanza na education. Katika maneno ya mashule, ni maoni yangu ya kwamba Constitution ipatiane nafasi ili kuwe na elimu ya bure kuanzia standard one mpaka university na ikiwezekana, ikiwa kuna mahitaji mengine ambayo yatahitaji kuchangiwa, Constitution ipatiane nafasi ya kwanza kwa orphans, watoto ambao hawana wazazi na masikini kuanzia grass root, labda kila sub-chief waweze kujua kuna orphans wangapi na hali ya umaskini pale na apeane majina ili watoto wale waweze kupatiwa elimu na wachangiwe kwa mahitaji mengine bure.

Na katika maneno ya shule, mimi pia ningesema ya kwamba, ikiwezekana, kila shule iwe na department ya guidance and counselling. Kila shule kuanzia primary, secondary, university, ziwe na department ya guidance and counseling ikisimamiwa ikiwezekana na kiongozi ama pastor ambaye amehitimu katika masomo ya counseling asimamie upande wa hiyo department. Na ikiwezekana, apatiwe nafasi ya ku-guide mwalimu mkuu katika hali ya canning. Iwe canning kwa kweli inaweza kuwa shida hapa na pale lakini baada ya counseling, apatiane guidance mwalimu mkuu mtoto mgani anastahili canning, mtoto mgani anahitahili guidance, mtoto mgani anahitahili counseling, mtoto mgani anahitahili kuongelehwa na mzazi, iwe ako na roho hiyo katika masomo.

Na katika upande wa pili ningetaja juu ya land tenure. Kwa mfano ingawaje imezungumziwa, ningesema ya kwamba katikati ya katiba tuwe na nafasi na proper description of the family unit. Family unit iwe properly described kwamba ni baba, mama na watoto. Na ikiwezekana, katika registered property za jamii, ziwe joint. Kwamba, kama ni mzee ako na bibi na watoto, yule huenda akafariki kwanza, asiachie wengine taabu. Wawe directly katika all registered properties, kama ni mtoto na amefikisha miaka kumi na nane awe partaker au awe jointly pamoja na mzazi ili baadaye ikiwa mmoja atakuwa deceased, yule ataachwa aweze automatically bila shida, kuweza kuangalia mali ya mzazi. Na pia pale, ikiwezekana, kwa sababu kuna watu wengi wenye uwezo na shida inakuwa land. Kuna watu wanakaa bure kwa vile hakuna mahali ya kulima, kuna watu wanakaa bure kwa vile hawana shamba nzuri za kulisha. Ikiwezekana kuwe na limit, iwe kila mwananchi asipate zaidi ya, ikiwezekana, heka mia moja za ardhi ili hata kama ni kununua, ikifikisha kiasi hicho, ile ingine iko juu, iwe ni ya serikali na serikali inaweza kugawia wananchi ama jambo kama hilo.

Ile ingine ningependa kutaja, ni juu ya judiciary ama makesi. Constitution ingefaa sana kama ingeonyesha mambo ambayo ni basic. Mambo yale ya chini kama vile mambo ya ndoa, na mambo ya land, na mambo ya crime, na mambo ya riots na yale mambo basic, Constitution ipatiane nafasi katika kila location ama sub-location tuwe na muungano ama kamati za viongozi wa makanisa. Ili badala ya kupeleka, kama ni mtu amekufa, na anatakikana kuzikwa na hajulikani atazikwa na nani, badala yakupelekwa kotini, kwanza, hawa viongozi wa makanisa waangalie na wapatie courts recommendations kwa sababu, kila wakati mtu anapofariki, hapo ni rahisi upate mtu wa kanisa, kama jamii iko na shida, utapata mtu wa kanisa karibu na ni rahisi aweze kujua kiini cha ile shida. Na ikiwa atashindwa na kuwa na solution, Constitution ingepatiana nafasi, hawa watu wa makanisa wawe wa kwanza kusikiliza na hata kama hawatatua, ikiwa mwishowe wataenda kotini, wapeane recommendations zao kwa koti.

Na pia kama vile mnenaji mwingine alisema, kama katika nchi zingine, dini imepatiwa umuhimu wa ku-guide society na utakuta katika nchi zingine, kuna sheria law na dini iko karibu sana na wananchi. Pia katika nchi yetu na sasa community ambao tuko hapa, tuseme Kathiani, ni community ambayo sana sana ni ya kikristo. Constitution ingepatiana nafasi ili ukristo uwe na nguvu na uweze kupatiwa nafasi katika Judiciary. Iwe kunaweza kuwa na kamati ya church Ministers ambao wamehitimu, kwa sababu kuna church Ministers ambao wamehitimu, iwe wanaweza kuwa na kamati kuanzia katika location na kusikiliza mambo mengine ambayo wanaweza kupatiana guidance hata katika koti. Kwa hivyo, Judiciary ingeangalia sana ama Constitution ingepeana nafasi ili kuwe na nafasi ya wachungaji na viongozi wa makanisa waweze kupatiana mwelekeo katika mambo mengine ambayo yanahitaji kuangaliwa kupitia katika hali ya kiroho. Kwa sababu wakati mwingine, mtu anaweza kupelekwa kotini na akuwe mbaya zaidi, iwe shida yake sio yale makosa alifanya, lakini shida yake ni kiroho. Na kwa hivyo kama hiyo ndiyo shida yake, kufungwa hakutamsaidia, lakini kukiwa na kamati kama hii, inaweza kuangalia ni jinsi gani inaweza kusaidia watu wa jinsi hiyo, kwa sababu kusudi ni kufanya mtu awe mzuri sio kumuharibu zaidi.

Jambo lingine ningetaja pale ni juu ya tax. Kodi ambayo tunalipa kwa central government na, ambayo wananchi wanalipa kwa local government ama kwa county councils, Constitution ingepatiana nafasi ama ingeacha mwelekeo ya kwamba, kila kodi

inalipwa na mwananchi ijulikane inayolipwa kufanyia kazi gani. Na hakuna nafasi mwananchi aweze kujua kama hiyo kodi iliingia katika kazi hizo, na ikiwa si hivyo, Constitution ipatie mwananchi nafasi ya kukataa kulipa kodi ikiwa haikuingia katika jambo lile ambalo lilikusudiwa. Na ama kushtaki the specific authority. Ikiwa ni county council, Mwananchi wa kawaida apatiwe nafasi ya kushtaki county council ikiwa hawaleti maendeleo kama vile vilivyo ama kama vile vilivyo andikwa.

Ile ingine ni farming - Katika hali ya ukulimaji, nchi yetu na community hii ambayo ni community ya ukulima kwa vile hakuna njia ingine ya kuleta mapato isipokuwa katika hali ya ukulima. Na hii ni sehemu nzuri ambapo kahawa inatoka vizuri na french beans na matunda na vegetables kama vile nyanya na kadhalika, na zinatoka vizuri na kwa wingi, kwa wingi zaidi kulingana na vile zimeangaliwa. Lakini kidogo ni kama haisaidii kabisa, na mwananchi imefika mahali, anaona hata afadhali asilime kabisa kwa vile nyingi za mapato ambayo inatoka katika ukulima, yanaharibika. Hata mahindi yanayotoka kwa wingi yanaharibika. French beans kwa wingi, zinaharibika, na nyanya na matunda mengine hata kahawa sasa ni kama haina kazi.

Comm. : Tafadhali tuende haraka.

Rev.Gideon Mbithi: Ok. Ninge-recommend kama Constitution ingepatiana nafasi ya serikali kuwa na reserve, ya kuweza kununua mapato ambao wananchi wanatoa. Wanalipa wananchi na serikali wanatafuta market ya kuuza.

Ile ingine ni jua kali artisan - Constitution ingeweka mkazo kwa hii ili katika kila kijiji kuwa na nafasi ya wale ambao hawana masomo, waweze kuwa na production katika hali ya jua kali production.

Ile ingine ni sand harvesting na mineral water. Hizo raw materials ni plenty. Kwa hivyo Constitution ingepatiana nafasi ya jinsi serikali inaweza kusaidia ili those commodities ziweze kuwa developed tuweze kuwa na kiwanda cha kutoa maji, Mineral water kwa vile it is natural and it is plenty, na labda serikali itupatie nafasi ama kiwanda ambacho kinaweza ku-develop sand ambayo also is plenty. Ile ingine ni katika hali ya uchumi. Lakini ndiyo hiyo nimetaja.

Ile ingine ni katika hali ya siasa, politics - kama ingewezekana, Constitution ingeweka nafasi katika kila polling station ambayo inaandikisha watu na kura zinapigwa, kura zihesabiwe hapo na wananchi waelezwe on the spot zile results za their polling stations. Kama ingewezekana pia Constitution apatiane nafasi kwa provincial administration kuanzia sub chief mpaka P.C., wachaguliwe na wana nchi na wapatiwe term, kama five years term. Na mayor wa towns na chairmen wa councils wachaguliwe directly na wananchi. Na katika hali ya afya, Constitution ipeane nafasi kwa kila mwananchi apate matibabu ya bure. Basi ni hayo, asante.

Com. Kangu: Thank you. Asante basi reverend, weka sahihi nafikiria tumsikilize bwana D.O kabla hatujaenda break ndiyo turudi na kuendelea na wengine.

D.O: Honourable Commissioners, honourable Kyalo Kaindi, M.P. Kathiani, wale wote leo wamefika hapa, kwanza kabisa yangu ni kuwashukuru Commissioners, tunajua muko na kazi ngumu.

Com. Kangu: Mention the names.

D.O: Nitashukuru kanisa kwa sababu tunajua munaendelea kufanya kazi muhimu ambayo pia ni ngumu. Pia ningependa kushukuru mweshimiwa wetu ambaye pia siku ya leo ako na sisi. Pia ningependa kushukuru wale wote wamefika hapa leo kupeana maoni yao kwa sababu wakati tulijua siku ya leo munakuja, mimi mwenyewe pamoja na coordinator na ofisi ya chama ya Constitution al review, tuli publicise ndiyo leo wameweza kufika hapa, kwa hivyo ningependa kushukuru wale wote wamefika.

Pamoja na hiyo ningependa tu kuongeza mambo mawili, matatu. Moja ya kwanza ni violation against women or may be domestic violation. Hii hasa imekuwa ngumu sana kwa akina mama kwa sababu tunaona wakina mama saa zingine wanachapwa na wanaume na zaidi. Kuna zile zingine labda tunazichukua kama ni assault au kwa njia ingine lakini nyingi inawachwa pale nyuma, ikichukuliwa tu lightly maybe a problem between a man and a woman. What I am suggesting is that, any violation against a man or a woman, hii domestic violence, haya maneno ya kuchapa should be taken seriously and illegal, should be taken as an assault. Kama ni kidogo kama ni kubwa, it should be looked at seriously. If it is an assault, it is an assault. Kama mtu amechapa bibi yake, kama amechapa labda mama mwingine au mama amechapa bwana au mtu mwingine, all of it should be assault. But what I have in mind is actually the one against women.

Then we also have rape, which is becoming actually a problem kwa hii Kenyayetu. Sana sana tunapata wanaume waki rape wanawake, labda hata wanawake pia sasa, wanaweza ku rape labda watoto au wana induce watoto wadogo wanaume. So what I feel is that we are giving a very light sentence kwa hawa watu. Sometime you might go into testing them for HIV and probably give a heavy convict. But what I am suggesting is that, these rape cases should not be taken lightly, it should be actually given a sentence which is equivalent to a murder case because if you can see a man who is HIV positive then rapes somebody and he is given a three years or seven years sentence, then all of them will die finally, I think this one should be taken seriously and be considered as a murder, whether the man is HIV positive, whether the woman is HIV positive or not, we should form an equal kind of sentence which should be equivalent to that one of murder.

Then the other one is a police power, especially the power of prosecution in that the police are the ones who arrest may be suspects and then take them to court for prosecution. What I am suggesting is that we should have an independent body whereby if a police officer arrests them, then they should be handed to that kind of authority or body together with the suspects and they charge them. Then this body should look and then take them to court. We know the court is there as an independent body standing between the police and the suspect, but we should have in mind that when a police officer takes them there, at any cost, they would like to win the case, that means they are very much biased. So I think we should have an independent

prosecution body.

The issue of the street boys. Actually it is becoming security and also environmental hazard. There should be a provision for these street boys seriously.

The other one is also parliamentary powers. We know that Parliament is the supreme law making body but we should not make them extreme. I think there should be a body or rather even a Commission, which should look into some of the things they pass. Some of the issues might be touching the nation very much and the passing of those issues might be politically instigated. So I think there should be a body, whether it is a court or a Commission, something should be there to counter check some of the things which may appear abnormal. Especially when it comes to their terms, like the salaries, now they have actually awarded themselves a very high salary when people of Kenya are being retrenched. I think there should be a body which should be checking some of these things. Even the law itself, now our worry is that if the Parliament refuses to accept even the Constitution now we are proposing, then what is going to happen is a disaster which may arise. I think something should be there to counter check some of these things.

The other one is HIV aids which is becoming a disaster in this country and all over the world. The Kenyan government has really tried by forming even some Commissions, some committees at all levels, but it doesn't seem to do a lot of work because the epidemic is still spreading and it is also destroying. We are very much worried. And what I am suggesting is that we have the public health act which is already there under which also may be the HIV falls as an health hazard. But I am suggesting that there should be a supplementary kind of act which should be in place to deal specifically with this HIV AIDS situation then I think we will be able to address the problem squarely and we will be able to save this nation.

Finally is the civic education - It is very much important for actually the community. Even right now as we are trying to bring our views, our problem is that we may have not much education about what we are trying to talk about. I think there should be a civic education system in place all through such as people will be taught, this is what is wrong according to the Kenyan law, according to Kenya Constitution and this is what is right. At least some basic education which should be in place such that when we take people to court, this principle or this idea of ignorance, not being a disease of course we say that ignorance is not a disease, but if we have been teaching our people on some life issues, then we can also justify that ignorance should not be defence because some of them have been enlightened. I think that is all I have.

Com. Kangu: Ngoja kidogo.

Com. Asiyu: D.O., I wanted to ask you one or two questions. When we were in the other constituency the Member of Parliament told us that the Provincial Administration stop people from coming to ask to give us their views. And in fact, on that same day the chief had called a baraza next to where we were receiving views and there were a lot of complaints about the

Provincial Administration not being very keen on this process. Today it is the opposite; we are seeing chiefs and the assistant chiefs and you in particular giving us your views, which are how, it should be. Why should there be such a big difference between one constituency and another?

Number two, you have made some very strong recommendations about violence against people, about rape and about police arresting prostitutes who I believe are usually women yet no one person can prostitute without the other. And we do not know why these policemen don't arrest men prostitutes; they seem more to be arresting women prostitutes. How can we help, what would you like to see in the new Constitution that would result in the police not harassing people but being helpful to them. We were told this morning might be you were not here, that you see a policeman you see death, you see a thief and you also see a rapist. This is the eye of the beholder, the way the people now see the policemen. What are your recommendations because in your position you should be able to help us so that we know what to put down as our recommendations in the Constitution.

D.O.: Yes, I think the differences within the divisions of the constituencies I think those are probably regional issues or difference or personal issues depending on may be the leaders and how they take. But I think for us, Kathiani division, we have decided to come and present our view that is our position. And then as far as I think, the policing issues are concerned, actually somebody has also said that the low salary is also a problem, that is why probably people go into corruption. I think there should be also, by the way Madam I said, police taking suspects on a brutal process, but there should be disciplinary measures which are in place and I hope the government is already doing something, the Commissioner of police is doing a lot, such that sometimes we find even people being interdicted or may be taken to court on the spot. I think that one should be encouraged.

Then there should also be a guidance and counseling. There should be also may be regular courses and also may be salaries, allowances and other remunerations. I think it is also better for that one to be looked at.

Com. Kangu: I have a specific question bwana D.O. First of all I want to comment you for this kind of a scenario where you have come forward to give us views. And you are not the only one, even when we went to Kipini, I think the D.O was (inaudible) so I think these are personal differences.

I have got two questions may be I want you to clarify. You have said street children are becoming a security and health hazard. What do you recommend the new Constitution to do? That is one point.

Number two, you have also commended on civic education, how do you want us to improve on the deliverance of civic education to all Kenyans knowing that about 70% of our people are illiterate.

D.O.: I think on the civic education, I am suggesting that probably there be a body attached to Judiciary, which should be there. And then they will be able to go round may be the districts, and they should be there existing even in the districts and may be even at the court such that these people when they are there, somebody must not even need to go to even necessarily

going to a lawyer. But might be able to go to an office and might be able to get some clarifications. They might go may be around the districts and then they be able to tell people exactly how the Constitution and the law of Kenya looks like especially at least the basic ones. They should be given this one in the language they understand. Vernacular language, the law should be interpreted even into vernacular languages and it should be able to reach the farmers. So just like any other employee or civil servants, these people should be there to go round and teach the public.

And then also on the street children, we are aware that there are these probation offices. We also have these NGOs and the other charity organisations, which are really trying to look into the matter. But what I am saying is that, I think the government should come forward in a stronger manner to ensure that the plight of these children should be taken care of. We do not like to seeing these boys on the streets in a miserable situation.

Com. Kangu: Thank you. Bado mumeweka bwana D.O katika waiting?

D.O.: No, I think we are through with you.

Com. Kangu: Thank you bwana D.O.

Comm. Kangu: Tunaona watu wamekuwa wengi na ninafikiria ile break tulikuwa tunasema tukienda tutapoteza muda. Tunataka tuendele, may be two of our colleagues can go, when they come back the others go so that tusifike jioni na watu wengi hawajasikizwa. So tutaendelea tusikize Mary Masibe. Mary Masibe yuko? Kama hayuko, Joyce Musau. Kama hayuko Beth Kitheka. Na kama huyo hayuko, tusikize Mwenda Mwanzia? John K. Konzo, businessman. Yuko ama hapana? Henry Muli, mwalimu Henry Muli. Where are they all these teachers? Then Mwalimu Mulwa David. Joseph Wambua, assistant chief Joseph Wambua. Sawasawa, then John Wambua, mkulima. Samuel Kitili, Mkulima. Haya, kuja bwana Kitili. Basi tusikize bwana Kitili. Please, tunyamaze tumsikize bwana Kitili. Samwel Kitili.

Samwel Kitili: Niko hapa.

Com. Kangu: Basi tusikize wewe.

Samwel Kitili: Ninasema ni asante sana ma Commissioners, wa

Com. Kangu: Anza kwa majina yako kamili.

Samwel Kitili: Jina langu naitwa Samwel Kitili. Ninasema asante sana kwa Commissioner na kamati yake. Na yangu ni swali moja. Watu wameongea hapa mambo mengi sana, yale yanahusu watu. Lakini kuna kitu kimoja, sijui serikali inasahau ni nini?

Au ni namna gani? Kuna kitu kimoja tuliletewa na mzungu kutoka zamani. Yaani, mzungu, sijui kama muliangalia vile mzungu anaona?

Com. Kangu: Wale wanazungumza wakati tunamsikiza mwenzenu, tafadhali msifanye hivo. Kama unataka kutoka nje, unatoka polepole bila kuleta kelele nyingi ndio tumsikize bwana Kitili. Endelea bwana Kitili.

Samwel Kitili: Na mzungu zamani wakati alikuja nchi hii, alizunguka yote akaona taabu ile utapata watu baadaye. Na akasema, atatafuta mti ile inaweza kuwa mzee kama mimi na bibi yangu au inaweza kusaidia watoto wetu kwa sababu kama una watoto na hauna mambo mengine ya kukusanya pesa. Kwa hivyo, nilikuwa ninauliza Commissioner, kuna kitu moja kinanisumbua lakini sijui ni kwa nini na serikali iko. Na nyinyi ndio mnapeleka ripoti ya kila watu na taabu yao, ipi na ile na ile. Kuna mti wetu hapa tunalima na unaitwa kahawa. Na hiyo ndiyo ilikuwa inasaidia mzee kama mimi na bibi yule hana bwana na mtu mwingine kama yule hana nguvu. Kwa sababu tukivuna, kuvuna haina taabu, lakini tukipeleka kwa machine kule, pesa yenyewe, inapotea huko hata sisi tunashangaa ni kwa nini. Hata ndio mimi nilikuwa ninauliza Commissioners. Haya mambo ya taabu yote, mulikuwa munapelekwa seminar na munaambiwa vile msikize taabu za watu, hiyo tutafanya nini? Kwa sababu mwaka huu, watu niliona hawataki kulima kahawa kwa sababu wanasikia ni kama dangerous kuchukua pesa yote, eti sisi watu wa Kathiani hapa, wanatuambia pesa inaenda na bank na hiyo bank hatujui ni nini? Na pesa zingine zimeliwa na watu binafsi na hiyo ni mali yetu na baada ya serikali kumfuata na kumwambia vile mzungu alikuwa akiweka. Kwa sababu siku hii, mzungu zamani alikuwa anaweka, kama unadaiwa utachukuliwa mali yako, au utapigiwa kithitu ndio ikumalize kwa sababu huyo mtu hana nguvu siku hizi. Hiyo ndiyo mzungu alikuwa anaona ni rahisi kwa mtu yule hana nguvu. Kwa hivyo mimi ninauliza, hiyo kitu utafanya naye nini? Itabadilika namna gani?

Com. Kangu: Lingine?

Samwel Kitili: Nyingine, sisi huko kwetu, yaani hapa area hii, tuna taabu nyingine. Unaona sasa tuna MP, Sasa tuko naye hapa na kama wakati unaweza kuwa mtu anaenda (inaudible) kufukuzana, atuambie nyinyi munafanya hii, munafanya hii kwa sababu D.O yuko huku. Mnaona kama hiyo kulipa tunaliwa wakiwa hapa, na munaona wale watu wanakula sisi na hawataki kurudi hapa watuambiye, nyinyi munasumbua watu wale hawana nguvu, lakini kwa sababu ujuzi uko mbele yao ndiyo tunawapeleka namna hii, namna hii, ndiyo hawa watu wapate ile kitu yao. Sasa hapo, tutafanya nini? Hayo ndiyo maoni yangu.

Com. Kangu: Asante basi, jilandikishe pale mzee wangu. Na tusikize Zacharia Kimeu, Hayuko? Paul Muli, karibu bwana.

Paul Muli: Asante sana, mimi nimeshukuru siku hii ya leo kuongea mada zangu juu ya hii kamati ya marekebisho ya katiba.

Com. Kangu: Tuambie majina.

Amendment ama kugeuza- katiba iliyoko ni nzuri lakini vile imekuwa ikigeuzwa imekuwa ikigeuzwa vibaya kwa kupendelea labda mtu fulani na tuna ushahidi kuna wakati mwingine ilifanywa kwa dakika hamsini kwa sababu mtu mmoja alikuwa anapendelewa. Tungependa ikiwa kuna Constitutional amendment kuwe na sehemu mbili. Kuwe na ile sehemu ambayo inaweza kufanywa na Bunge peke yake, wakati wanapenda kuwe na sehemu zile ambazo haziwezi kufanywa na Bunge kabla hazijapewa wenyeji wakazichunguza. Kuwe na referendum, ifanyiwe recommendations by Parliament.

Ile ingine ni Legislature, kuwa na chamber cha Bungetumeona madhala yake sababu wakati watu wanaozungumzia kitu wa kiwa pamoja wanaweza kusahau pande zingine. Kwa hivyo ningependa warudishe ile sehemu ilikuwepo ya kuwa na chamber cha pili.

Kile kingine wale ambao watachaguliwa kwa bunge, ningependelea wawe na minimum qualifications si ati kila mtu anaweza kuenda Bunge kwa sababu siwezi kwenda kutengeza sheria na mimi sijui lugha na sijui kile kina ongelewa huko. Mimi ninaenda huko kuharibu wakati wa wananchi. Kwa hivyo tunataka kuwe na qualification per person zile zingefuatwa wakati

mtu anapatiwa kiti cha kwenda Bunge.

Com. Ayonga: Na hizo qualifications ni gani?

Munyao: Ningesema mtu awe amefanya mpaka kidato cha nne huyo mtu anaweza kuwa mbunge.

Kile kingine ni katika representation in Parliament. Tumeona na tunashangaa katika Bunge unakuta mbunge anasimamia watu elfu kumi na mtu mwingine ana represent watu elfu mia moja kwa hivyo unaona hiyo representation is not propotional. Tunge penda watu wafanyiwe representation in Parliament propotionally ikiwa tuseme constituency yetu iko na watu wengi iwe na wajumbe wengi, ikiwa iko na watu wachache iwe na wachache, kwa hivyo kuwe na provision katika Constitution inaonyesha mjumbe mmoja anafaa watu wangapi kama kwa mfano hapa Kathiani tuko na watu karibu elfu mia moja. Huyo ana ongea watu elfu kumi na huyu watu elfu mia moja, hiyo haifai.

Ile ingine ningesema katika nomination to members of Parliament wale wanafanyiwa nomination, nomination nayo pia ifanyiwe na proportion age representation in Parliament iwe ile chama ilipata watu wengi pia ipatiwe watu wengi. Na hii nomination isifanyiwe tu mtu kuonekana lakini awe hana kazi anafanya. Ningependa public service ifanyiwe representation in Parliament wakati wa nomination, organization zipatiwe representation in Parliament, union wapatwe representaion, minority groups wapatiwe representation. It is a wonder we have minority groups in Kenya who will never see Parliament if we go by the way we are going. We have the Asians, they are Kenyans and they need the representation. We have the disabled and the disadvantaged. We need to have these people represented when nomination is being put into consideration.

The other thing is about Parliament having a permanent timetable. We need to have a timetable one, which start from election to dissolution of Parliament. Hakuna mtu anaweza kuwa ana uwezo wa kuvunja bunge. Bunge iwe inajivunja yenyewe na Katiba. Tunajua tumechaguana leo na tunajua hii Bunge itamaliza kazi yake mwaka fulani siku fulani.

Ile ingine citizenship, we are loosing very useful resources from our people, human resources, that is what I am saying. Wakati mtu anakuwa Kenya anaenda anakuwa raia wa Denmark, kama tunajua wakimbiaji, anaenda kuwa raia wa America kwa sababu Kenyayetu haina provision ya dual citizenship. Huyo mtu hawezi kuwa mkenyatena. Anaacha kuwa mkenyana ni wetu. Kwa hivyo ningependelea ikiwa kunawezekana tuwe tunaweza kupatia watu wetu, wanaweza kuwa citizen wa nchi zingine na wanaendelea still kuwa citizens wa Kenya.

Kile kingine ni shida ya citizenship inaweza kuingia. Ninaenda America au mtoto wangu anaenda America na aoe huko. Akioa huko masharti ya yule bibi yake kuwa mkenya inakuwa ngumu, kwa hivyo inamfanya huyo mtoto wangu hajifanye mwamerica badala ya kurudi Kenya. Kwa hivyo ningesema ikiwa mkenya anaoa mwanamke kutoka nchi ingine, huyu mwanamke anakuwa automatically Kenyan citizen if the marriage is legalized in Kenya

Ile ingine ni political party mandate and defection, we are fed up with our politicians. Mtu anasimama kwa Bunge anasema mimi leo sita kuwa wa chama kile kingine kilichonichagua na anaendelea kukaa kwa bunge, huko ni kutusi wale waliomchagua. The law is there which says ni lazima huyu mtu aandike kwa bunge, andikie speaker. Tunasema provision ya katiba iseme, mtu akiongea adharani hata ikiwa ni kwa soko hapa Kathiani akisema sasa sioni maana ya kile chama kilichonichagua iwe ni verbal, iwe ni written, ikisha ingia kwa wananchi huyu mtu kutoka saa hiyo anaacha kuwa mtu amechaguliwa na badala yake kuchaguliwe mwingine sababu wengine hata karibu nusu ya Bunge tulionayo ni ya watu watoro waliotoroka vyama vyao. Kama ni katika merging ikuwa ni merging, mki-merge vyama viwili, chama kile kidogo kilitaka kimezwe na kile kikubwa wale wamemezwa mara moja wanapoteza ubunge wao, warudi kwao wakachaguliwe tena hakuna haja ya mtu alichaguliwa na watu na anageuka anaingia imani hii anaendelea kuwa still mbunge.

Com. Ayonga: Maliza sasa mzee,

Munyao: Unajua nilikuwa na vitu vingi vya kusema lakini viko hapa. Ile ya mwisho ningependa moja, ni habari ya retirement. Kama ninaona hapa mbele yangu kuna mzee mwenzangu umesha- retire najua. Wakati una- retire unakuta mtu anaenda nyumbani na anakaa miaka miwili bila kupata benefit zake na unashangaa kwa nini na huyu mtu wakati alikuwa anafanya kazi, employer wake alikuwa anajua huyu mtu ataenda nyumbani. Kwa hivyo ningesema hivi wakati unafiikia wakati wa retirement benefit zako zina fanyiwa preparation unazipata wakati unapoondoka, usiwe unaambiwa uongojee. Ziwe zinakuwa automatic na zinaingia.

Com. Ayonga: Asante, si umesema hiyo ndiyo ya mwisho tafadhali tupe hiyo karatasi na asante kwa maoni yako. Now, yule mwingine alikuwa nani? Wewe ni nani? chukuwa mic, mzee umesahau tupe mic yetu, iko kwa mkono wako. Sasa wewe tupe majina yako ukitumia hiyo.

Julius Kitavi: Majina ni Julius Kitavi, kitu cha kwanza unakuta siku hizi umesomesha mtoto na umeuza kila kitu na ukienda mahali popote kwa ofisi kuuliza kazi unaambiwa toa chai kidogo na you have undergone up to diploma level, and you have nothing in the pocket to give that particular person. Something of that sort should be followed by the government for those people who do such things.

Ya pili, ni juu ya colleges. Unakuta college zingine unaendelea na unambiwa hakuna kazi watu ni wengi, hakuna kazi unaweza kupata especially now days waalimu. Unamaliza course ya ualimu na hakuna kazi, ukiuliza unambiwa hata wengine wanaenda, wanafutwa kazi na wewe ndio umetoka college na hakuna mahali utaenda, so our government should think after college where we should go and what we should do because now days they are taking us to colleges, you complete the college, no job no matter whether it is university level, you go to university up to diploma level you find there is no job.

Com. Ayonga: Tafadhali wale wanaongea wanaweza kwenda kuongea nje maneno yenu tuwe na baraza moja.

Kitavi: So our government should, if not so I think the education in Kenya now days is going down because there is no need of unasomesha mtoto anamaliza shule, umeharibu kila kitu na unaambiwa hakuna kazi.

Com. Asiyu: Tunataka utuambie kwa katiba tuandike namna gani mambo hayo

Kitavi: They should have a change especially the working systems. These years of working should be reduced they are many because you find some of them they are working more than forty up to fifty years and the government is not aware of these people.

Com. Asiyu: Thank you, unaweza kujiandikisha jina kule, sasa ni huyu mzee, sema majina yako.

John Kirio: Nitaongea kidogo tu, kwa hivyo mimi yangu ni habari ya elimu, elimu ningetaka iwe ni ya bure kutoka nursery mpaka university na hata course za waalimu zote, ziwe ni za bure, zilipiwe na Serikali.

Ile ingine ni habari ya hospitali kutibiwa, ningetaka watu wote wawe wakitibiwa bure ata wale wanalazwa hata maiti iwe ikichukuliwa bure si kulipishwa.

Ile ingine ningetaka katiba iandikwe kwa lugha zote zile ziko Kenya ili iwe inafahamika na watu wote. Sina lingine.

Com. Ayonga: Asante mzee umetupa mambo ma tatu, elimu ipatikane bure mpaka university, hospitali watupe free treatment. Kulikuweco wale nyinyi mnakaa hapa wewe unataka kuongea? Uje?

Joseph Mulu: Asante kwa mwenye kiti, mimi ninaitwa Joseph Mulu Mwasia. Yangu ninaongea kuhusu human rights. Mimi kama mkenya natoka hapa naenda Busia, naenda Mombasa, nikinunua shamba huko na pesa zangu nauziwa baadaye kuingia kwa ingine wanasema huyu ni mtoro hawezi kuwa ni wa shamba hii na mimi ni mkenya na nimelipa pesa yangu. Mimi nilikuwa nafanya nini wa.... Mimi nauliza, mimi natoka hapa kama mkenya

Com. Asiyu: Hiyo tumesikia. Unapendekeza namna gani?

Mulu: Napendekeza kila mkenyaakienda pahali popote, akinunua sehemu awe mtu wa hapo bila kuambia ati wewe ni kabila hii.

Ya pili, naongea juu ya mashamba na wale wanauza na wanunuaji. Mtu anaweza akatoka hapa anaenda mbali ananunua shamba na hiyo shamba iwe imeuziwa mtu mwingine, kwa mteja mmoja, ndio nauliza hiyo katiba irekebishwe iwe mnunuaji ni mmoja si wawili.

Point ingine ni upande wa security. Inafaa kuwa upande ya serikali kwa office za Serikali, sababu mwenye kiti wa central ...ndiye anajua mambo ya security upande wa district, provincial ndio office ya Rais inawekwa. Mimi ninaunga mkono ile iko sasa.

Com. Ayonga: Asante asante sana kwa maoni yako enda kule ujiandikishe nani yule tena mwingine. Tafadhali tuwe kimya ili tuweze kumsikia.

Peter Nzau: Mimi naitwa Peter Nzau Mutua, kwa mapendekezo yangu ningetaka kuuliza Commissioner, ninajua imezungumziwa lakini nitazungumza. Free education kutoka nursery mpaka standard eight.

Ya pili, ningepili iwe pendekezo, administrators na chiefs wawe wakipewa transfer kama ma-officer wale wengine wa serikali.

Ya tatu, ningetaka kupendekeza local government ile ambayo inachukua revenue kwa soko yoyote kuwe na Commission ya pesa, kiasi fulani za kuendesha area hiyo pesa zinatoka. Nimemaliza.

Com. Ayonga: Asante sana Peter Nzau, unaweza kuenda kule ujiandikishe na huyo aliye kuwa karibu sana, huyu ambaye anasimama tena anarudi kwa kiti wewe kuja ndugu yangu kama uko tayari. Si wewe ulikuwa unataka kuongea na mbona nikikulenga hutaki kuniangalia? wewe endelea. Tafadhali huyu akimaliza you are next.

Joseph Musyoka Muindi: Asante Commissioner, majina yangu naitwa Joseph Musyoka Muindi. Nina maoni kidogo tu, na nitaguzia vile umesema tuguzie kwa ufupi. Kwa kweli sisi wana Kenya tuna shida wale ambao hawajasoma, pengine hata wale wamesoma kama sisi. Namba moja Katiba, sisi tukielezwa hali ya katiba hatujui katiba ni nini, sasa tungeuliza yenyewe tuelezewe katiba ni nini na ile lugha ambayo tungewza kujua katiba ni nini. Ikiwa ni uchaguzi au ni nini imeandikwa kule ndani ndio tuweze kuelewa mzee kama mimi katiba ni nini.

Ya tatu, vile ilikuwa zamani kama mwaka wa sitini kuja kufika mwaka wa sabini, kulikuwa kuna wakubwa ndio hatukatai na kukawa na wadogo na maduka yalikuwa ya watu wakubwa na maduka ya watu wadogo lakini tunge fuatilia pale ndani kwa wazungu, tukakuta wakubwa wako na mshahara mkubwa na wanarudisha kwao pahali ambapo wametoka ule mshahara mkubwa ambao ungepewa yule mdogo ambaye hajiwezi. Kwa nini Kenya hatuwezi kupendana namna hiyo ikiwa wazungu walipendana au vile wazee wa zamani walikuwa wanapendana?

Com. Ayonga: Maoni yako ni nini? Unataka tuandike nini kwa Katiba?

Muindi: Bwana chairman kama ningepilizwa maoni yangu unaweza kuwa na elfu mia tatu na mimi mtu wa chini kabisa niko na mia moja. Kweli tukiangalia undani hizo pesa kweli zinaweza kwa yule mtu ako chini yule ambaye hajiwezi mkulima.

Ya tatu Serikali, ndio tuna serikali na ambayo ni mtukufu Rais na ni President na vile tunajua tulikuwa na Gatundu baada yake. Kukawekwa stima, kukawekwa maji ya kunyunyiziwa tukawa tunasikia Gatundu. Je, hizo pesa huwa kwa serikali ama huwa ni za wenyewe kwa vile utakuta mashamba makubwa kwa huyu tuseme President yeyote utakuta kuna vitu nyingi kwa hiyo area tuseme kama hii Kathiani mmekuja, na ndio swali langu au maoni yangu mnijibu niweze kuelewa kwa sababu sielewi. Hiyo pesa huwa ya serikali au ya mwenyewe hiyo inafanya kazi area hiyo?

Ya nne, tuna-minister hapa kwetu na vile sijui kama imesemwa na mwingine pengine amesema na lugha ambayo sielewi, utakuta tuna Minister, sisi wananchi tumemchagua na ukitembea na ile kumchagua kwa ukweli utakuta haikuwa mapendeleo yetu kumchagua ni ile laini fupi ndio imepita. Je, huyu mtu hata hatujamuona, mtu hata miaka tano ikwishe hautakuwa umemuona na bado tunaambiwa ni mbunge, hata sehemu zingine hafiki. Tutajuaje huyu mtu anatutetea au hutetei kwa sababu hatumuoni hata hatumsikii.

Com. Ayonga: Lakini sasa mzee ebu nikuongoze, wewe ndio utuambie huyo Minister ambaye hujamuona kwa miaka mitano unataka tufanye aje.

Muindi: Si maendeleo, hakuna kitu kingine tunamtakia hatuletei maendeleo.

Com. Ayonga: inakuwa huyo mtu humuoni na ulimchagua na amekwenda miaka mtano hujamuona kwa hivyo unapendekeza nini?

Muindi: kama hatutoshelezi aseme kwa serikali tuchague watatu au wanne wawe wanaweza kutufikia.

Com. Asiyu: kwa kweli wewe unasadiki kuwa mjumbe kama huyu anaweza kwenda kwa serikali aseme yeye hawezi kufanya kazi aondolewa na Serikali?

Muindi: si kwa serikali ni sisi tumeshindwa sababu hatumuoni tumeshidwa sasa.

Com. Asiyu: kitu utuambie ni hii, nchi zingine wanafanya hivi kama mjumbe hawezi kufanya kazi yake kwa muda fulani, wananchi wanaweza kuka pamoja wakaandika memoradum wakapeleka kwa speaker ikionekana ni kweli hakuna fitina ndani ya hayo mambo kuna kitu kinaitwa sheria ya return, halafu anarudi mambo yake yanatengenezwa alafu mwingine achaguliwe lakini vile unaongea huwezi kutusaidia kuandika katiba wewe.

Com. Ayonga: Asante na dakika zako zimekwisha. Ya mwisho ni nini hebu nione

Muindi: Ya mwisho ni hasa sisi wakulima, tulikuwa tunauliza kama ingewezekana hii maji hata umepitia Athi River umeiona umepitia kila mahali, hii maji hakuna yeyote anatusaidia na inapita inatiririka na unasikia ukambani kuna njaa?

Com. Ayonga: na si mnasaidiwa?

Muindi: tunasaidiwa na upande ya hayo maji? pendekezo langu hayo maji kama yangehifadhiwa hayo maji tu tuyatumie wakamba tuwache kufa na njaa.

Com. Asiyu: Mungu atawapatia si ndio sasa wewe useme sisi tupendekeze mjengewe damu kwa ile river ishike dam kando kando ndio mpate kuwa na maji ya wanyama na ya nyumbani na ya kuweka irrigation. Sasa unatuambia mambo hatusikii.

Com. Kangu: Thank you umeuliza lakini Commissioner amekuambia ungalisema tunataka maji haya yazuliwe, ili yaweze kufanyiwa irrigation na wanyama pia yaweze kupata maji ya kunywa. Enda kule uandikishe jina. Sema majina yako kamili.

Moses Wambua Masila: Asante sana jina langu ni moses Wambua Masila. Jambo la kwanza la kusema ni hili la administration, tukianza na assistant chiefs. Mimi ningependekeza ya kwamba mtu kama assistant chief na chiefs hawa wangepaswa wawe wanachaguliwa na wenyeji kwenye wanawakilisha kwenye zile sehemu zao.

Ya pili ni sehemu zenye nimeona mzee mwenzangu amesita kidogo lakini pole kwa kusema hivyo. ni kuhusu ya hawa wabunge, ningeliza wabungekama hawatimizi matakwa ya watu wawe wanapigiwa kura ya kutokuwa na imani nao kwa vile wanaumiza wale walienda kuwawakilisha.

Inginge ni jambo la elimu, sasa haya maneno ya elimu saa zingine mimi ni mzazi na tunaenda tunaambiwa jambo kama vile President alisema jambo hili na hili lisifanywe. Watu tuseme kuanzia hawa ma-DO wanakuja wanakuwa na mipango ingine. Sasa huwa tunashindwa tutafuata nani kuna viongozi pale mwenye anatuambia vile tunaelekea, na kuna mwingine hapa anasema huyu President hayuko hapa maendeleo ni yetu, sasa hii inakuwa ni mvutano katikati ya sisi wazazi kwa vile tunaona kama kuna unyanyasaji katikati ya hawa wakuu wa elimu.

Com. Kangu: Kwa hivyo sasa tupe pendekezo lako.

Moses: Pendekezo letu ni wawe wana announce kila kitu kama President amesema kitu iwe amepitisha, kuliko kuja kuambiwa ati hapa President anajenga kwao. Kwa vile sisi tunaona saa zingine kuna hii activity, siku hizi tuseme wakati kama huu watoto wangali wanafukuziwa hiyi activity fee na President hiyo alipiga marufuku kabisa, sasa sisi tunashindwa hii inaenda namna hii, hii inarudi tena huku.

Ile ingine ya mwisho, mhesimiwa ningeliza ni hawa wabungetuwe tunajua hesabu ya mishahara yao, kwa sababu wengine wanajiwekea mishahara mikubwa na vile hawafanyi kazi. Kuna wengine hata tangu hiyo Bungeifunguliwe hawajaenda huko kwa Bunge tuseme masiku kama ishirini hivi na bado unasikia wengine wanalalamika wanalipwa more than five hundred thousand. Sasa unajua hiyo nikuchukua pesa za watu bila kufanya, kazi kwa hivyo hiyo ningeliza upunguzwe sana. Asante.

Com. Ayonga: Thank you

Com. Asiyu: Lakini unataka kutuambia Bunge kama mtu hajafika mara nne bila sababu yeyote, anaweza kupoteza kiti chake. Kwa hivyo sijui kama wanakaa siku ishirini kama hawajaenda bunge.

Moses: Hiyo sijajua na kuna wakati mbungewetu alikaa karibu hata karibu mihula tatu bila kusikia akiwakilisha area yetu.

Com. Ayonga: pengine alikuwa akifanya technical appearance, tafadhali ujiandikishe huko. Na tena wakati mwingine wewe fanya bidii uwe unaenda kule Parliament kuna gallery huko ambako unaweza ukaketi, ukaangalia wabunge wanafanya nini, uone kama huyu wako analala, anauliza maswali au anafanya nini. Katika hawa nimemaliza nataka kusonga kuna mtu hapa ambaye nimemuacha kuja. Lakini ndugu yangu your face is familiar.

Stephen: Thank you for this opportunity; my names are Stephen Nzui a teacher at Kathiani Girls. Honorable Commissioners and members I would like to kindly draw your attention to the following areas in the Constitution which call for review and if possible some amendment.

One, we have the Vice President. It is to the interest of the citizens that the Constitution provides that the Vice President be elected by the people during the national general elections that is the person who comes second in the result for the elections automatically becomes the Vice-President.

Secondly, we need a society in which social and economical justice is guaranteed, that is there should be a Constitutional amendment to make a provision for the government to set minimum salaries at all levels of employment that will curb the problem of exploitation over money. We also have basic education for all then for that the Constitution should have a clause which commits the government to take responsibility to ensure basic education for children where parents are unable to pay for it and for that I think that basic education is a human right.

Then there is public health, and for this the Act governing cost sharing in public hospitals need to be reviewed since some people are unable to pay the medical expenses. That is all I had.

Com. Ayonga: Thank you mwalimu ni kitu kizuri kuwa na walimu wakati mwingine wanapofanya summary na unaweza

kuenda kule ujiandikishe na kama hiyo karatasi yako unaweza kuwacha uache. Niliona mzee mwenye kofia. Lakini mtu mwingine anaonekana hapa, okey ongea kwa vile umefika, sema majina yako.

Twambui: Mimi ni former Councillor wa area hii vile vile mimi ni trade unionist wa zamani tangu uhuru mpaka sasa. Nataka kutoa tu mapendekezo kidogo kuhusu uchaguzi. Katiba tulio nayo sasa wakati huu kunachaguliwa President wakati wa uchaguzi, mjumbe, Councillor lakini wakati tunaanza kufanya kazi unakuta Councillor analipwa pesa kidogo sana na yeye ndiye ako hapa chini na wananchi na matatizo yote ya sehemu inaletwa kwake na wananchi ili aweze kuwasaidia lakini kama analipwa shilingi elfu tisa atasaidia nani? Ingelifaa kama kweli watu wamechaguliwa watatu malipo ionekane kulingana na uwakilishaji wa wingi wa watu. Kwa mfano kama saa hii nasikia wajumbe wanalipwa shilingi elfu mia tano, na constituency moja unaweza kukuta iko na ma-councillor wanne au watano, inafaa hiyo pesa igawanywe ile inalipwea mjumbe huyo kwa kusimamia constituency pesa yake igawanywe kulinganishwa na ma-coucilor ili ma-Councillor wale wako area yake walipwe, ile pesa ikilinganishwa iwe sawa na ile analipwa yeye mwenyewe.

Usimamizi wa Councillor au county councils na municipality. Utakuta ma-Councillor wanasemekana ndio wenye kusimamia, hao ndio wenye council kwa sababu without Councillor there is no council, lakini hawana uwezo wanaangaishwa na senior officers ambao hawana uwezo wa kuwafuta. Now, if you have given responsibility without authourity it is useless. Infaa Councillorswapewe uwezo wa kusimamia councils zao, wawe na uwezo wa kuandika na kufuta yule anayepatikana na makosa. Lakini kwa wakati huu unajua vile iko, huwezi kufuta clerk, uwezi treasurer kwa sababu hao wameandikwa na council. Ndio unaona council zetu zina kuwa na shida na mambo mengi kwa sababu ma-Councillorshawa uwezo wa ku-manage na kusimamia council hiyo. System yetu ya serikali mimi ningeunga mkono iwe ya vyama vingi, au ningependekeza iwe ya vyama viwili.

Pili, ningependekeza hivi President awe ceremonial President asiwe na uwezo kwa popote anaenda kwa mkutano anatengeneza sheria zake huko na inanza kufanya kazi wakati huo. Bungeinafanya kazi gani? Sheria zinafaa zitungwe na Bungena zile zimetungwa na Bungendizo zinafaa kufanya kazi lakini si sheria za kutangaza popote. Mtu anapoenda anasema hii kufika leo hii nimesema hii. hiyo haina ya system ya serikali kwa wakati huu tunataka kuwe na ceremonial President mapendekezo yangu, kuwe na Vice President, kuwe na Prime Minister , kuwe na deputy Prime Minister wawili.

Katika mambo hiyo ya system ningelipendekeza kujiandikisha kwa kura kuendele kama vile mambo ya vipande inavyoendelea bila kukoma.

Com. Ayonga: Mzee malizia.

Twambui: Yangu ni mengi sijui utanikatiza katikati.

Com. Ayonga: Kuna wengine ambao wamengoja hapa toka asubuhi mzee.

Twambui: Okey, umenikatiza sasa nimepotea. Hiyo nitawachia hapo. Niende kwa point ingine, ukimwi. Hii ugonjwa nimesikia mambo mengi serikali inalia nasikia mambo mingi juu ya ukimwi. Na mapendekezo yangu ni haya, kama inawezekana iwekwe katika katiba yetu wananchi wote wa Kenya wachunguzwe ili kujulikane wale wako na ukimwi ni wangapi na wale wasio na ukimwi ni wangapi. Na kama mwananchi wa Kenya anaenda nje akirudi tena anafanyiwa uchunguzi kama yeye pengine ako na ugonjwa huo, na ikiwezikana watu wale wanapatikana na ugonjwa hii ikiwezekana watenganishwe na watu wengine, kwa maana sasa unapona huu ugonjwa unazidi ni vile mnasema wapatiwe mapenzi, kuwe na hii kuwe na hii halafu wanaendelea kuongeza, ugonjwa unaendelea kuenea kumaliza vijana ambao wanatakiwa wajenge nchi hii. Kama inaweza kuwekwa hiyo ingekuwa vizuri.

Mambo ya kazi ya retirement - ningependekeza watu wafanye kazi miaka arobaini na tano waweze ku-retire katika public service au kwa private sectors, ili kupatia vijana ambao wamemaliza mashule na hawana kazi nao nafasi waweze kufanya kazi. Sasa katiba tuliyo nayo watu wanafanya kazi miaka sabini na wale wamesoma wanahangaika huku watapata wapi kazi kama mtu anafanya kazi miaka sabini. Ningependekeza miaka ipunguzwe.

Police wa AP- ningependekeza hiyo iunganishwe ikuwe moja. Mimi sioni haja ya AP, wakati anakamata mtu haendi kotini kumshtaki, anakamata na anapeleka kwa polisi, na ndiye anaenda kushitaki na inakuwa long process, wastage of money and time. Ingeliunganishwa iwe Jeshi moja, wawe wanafanya kazi moja, na hiyo inaweza kufanya mambo ya sheria inaenda karibu bara bara.

Nataka kupendekeza mimi mkamba. Sisi tuko na clan ama mbai na siku hizi imemalizika nguvu na ndiyo ilikuwa inasaidia serikali kwa kuweza kuadhibu watu kutoka katika boma ikiwa wanafanya makosa ambayo hayaambatani na sheria za Wakamba. Nami nafikiri makabila mengine katika Kenya wako na clans. Ningelipendekeza kama ikiwezekana clanism iingizwe katika katiba na wale watu wako na clan zao wapatiwe uwezo wa kuweza kuadhibu wale wanaokosa na wanaopotea njia kwa sababu siku hizi utakuta watoto hawasikii, hawaheshimu wazazi na hakuna jambo wanafanyiwa. Ikiwa tutaacha tu kuwa ati sehemu yetu ya sheria ndiyo itafanya kazi hii ndio unaona uhalifu umezidi na watu wengi wajeuri wametapaka. Kwa hivyo nipendekezo langu kama itakubaliwa iingizwe na ipatiwe uwezo kama vile ilikuwa.

Ya mwisho, hawa chokora au watoto wanaitwa chokora wametapaka nchi yetu wanatoka mji mkubwa sasa wanakuja huku. Hawa watoto wanaanza kunywa gum, bhangi nyingi na bado serikali inaona na sioni ile hatua inachukua. Ningelipendekeza hivi, watoto hawa wanazaliwa na watu, nataka katika katiba iingizwe mambo ya chokora kwa sababu miaka ijayo itakuwa shida sana kwa watu na ingelifaa iingizwe kwa katiba na serikali ichukue jukumu la kukusanya watoto wote wale wanaorandaranda katika sokoni na kuchunguza kweli kama ni chokora wa kweli wenye hawana wazazi. Wakipatikana hawana wazazi wajengewe, sitaki kusema jela au shule, wajengewe makao wapatiwe elimu huko

wafundishwe kazi huko wazuiliwe huko bila kuachiliwa na kuja kutangatanga na wasomeshe na serikali. Na wale wengine wakichunguzwa waonekane wazazi ndio wanawaachilia ovyo ovyo na wana uwezo wa kulea watoto wao, ningelipendekeza iingizwe kwa katiba hao wazazi walazimishwe kuchukua nakuangalia na kulea watoto wao. Na ikiwa serikali haiwezi kupata pesa za kuweza kugharamia gharama hii, ni heri au mimi napendekeza iongezwe hata kama ni sumuni juu ya kodi ambayo inayotozwa raia ili kuweze kupatikana pesa ya kuwalea na kuwasomesha watoto hawa.

Com. Ayonga: Thank so much mzee kwa maoni yako mazuri ambayo umetupa

Twambui: Mimi nilikuwa nataka kukaa masaa mawili nikitoa maoni yangu. Lakini naona wewe unanikazana.

Com. Ayonga: lakini kitu ambacho ungefanya mzee kwenda andika hatam ukiandika page kumi halafu uletee hiyo itaenda kuwekwa kwa computer maneno yako yote tumeshapata your main points.

Twambui: Sasa mimi nataka kuuliza swali sijui wewe utanijibu?

Com. Ayonga: Siulizwi maswali.

Twambui: kama wewe hujibu, maoni yangu ni hii, hii Commission ya marekebisho ya katiba, iwekwe permanent iwe inaweza kukaa baada ya miaka kumi inakaa tena kuanza kuchunguza maendeleo ile imefanywa na katiba iliyomaliza miaka kumi ili watu waanze kutoa maoni yao juu ya katiba mpya kubadilisha vigumu vigumu. Education hii sasa ya civic haikuwa nzuri kwa sababu hatujui katiba ni nini tunaambiwa kubadilisha katiba nitabadilisha katiba gani na ile ya mbele mimi sijui?

Com. Ayonga: Asante sana mzee kwa maoni yako.

Twambui: Kwa hivyo iwe na nafasi ili raia waweze kupatiwa civic education waweze kuelewa kubadilisha katiba ni nini na kutengeneza katiba ni nini.

Com. Ayonga: Asante sana. Wapi huyu, ni wewe, ndipo nitaanza list ingine. Tafadhali keti na chukua microphone, sema majina yako.

Paul Kamanga: Naitwa Paul Kamanga. Asante kwa mwenye kiti kwa kunipa wakati huu niwe nikisema machache kuhusu huu mkutano. Asante sana. Yangu ni moja ambaye ninasema hivi.

Tutaanza na shule - Ningelipendekeza mimi mwenyewe kama inawezekana kuanzia nursery mpaka university iwe ni line moja, masomo ya free.

Ya pili, nimesikia mtu mwingine hapa ameahidi ya kwamba kuna kitu kimoja ambacho kinaitwa pombe. Pombe, nitaongea kwa

kifupi kuhusu pombe. Hiyo pombe ambayo tunayosema hapa, ni pombe ya muratina kwetu lakini tukienda pwani huko siutakuta wagama na ukikuta wagama hao wagama ukiwakataza hiyo pombe ya kugema huko kwa minazi hawa si utawaua au wataweka kamba? Sasa ningependekeza mimi kwa maoni yangu sasa sisi muacha mila ni mtumwa na sisi hatutaki tuwache mila kwanza tunataka to follow mila yetu. Kuna pombe ile ambayo tunaenda kuoana na hiyo pombe. Nikipeleka zile mbuzi tatu unapeleka na pombe. Ukipeleka kila kitu kwa shemeji wako unapeleka na pombe. Sasa hii pombe mliyosema ni mbaya, inaweza kuwa ni mbaya kivipi?

Com. Ayonga: Wewe tuambie unatakaje?

Paul: Sasa ningependekeza hii pombe iwe kidogo lakini sio zaidi. Kwa kusema ukweli, mimi kwangu mimi, mwenyewe kuna gari ambayo imewekwa hapo na shetani hata sio mimi nimeweka mimi ile ya kusema ile ya kusaga miwa. Na hiyo gari iking'olewa hapo hata yule anakuja kung'oa hiyo gari yeye mwenyewe atakutana mashetani yake sababu mimi sio mimi niliweka hapo ndani iliwekwa na mwenyewe. Kwa hivyo ninataka waandike hichoo kitu.

Com. Ayonga: Gari gani iko kwako?

Paul: Iko gari moja ambayo ni ya kusaga miwa na hiyo gari mimi ninasaga miwa wakati ule nimeambiwa nisage miwa na hiyo shetani. Lakini sisagi kila wakati.

Com. Ayonga: Hebu tusikie haya maneno ya Paul ni mageni kwa wengine wetu pengine nyinyi mnaelewa kitu anachosema na tuko hapa kwa kusikia, tuelewe ni kitu gani Paul anasema tupeleke, kwa hivyo mtuachie nafasi ya kumsikia.

Paul: Kwa hivyo, hiyo gari ambayo vile nimeikuta hapo, sio mimi nilienda nikaitengeneza nikaiweka hapo, imeletwa na shetani hapo. Na sasa wakati ule mimi nimeambiwa nisage hiyo miwa kidogo ninaenda na nunua halafu nasaga kapombe kidogo alafu nakuja na wamwagia hapo chini ndio iwe kikao ya family yangu. Sasa mimi sinywi pombe mimi mwenyewe. Lakini hiyo pombe mnayosema, ninataka iandikwe isiwe nyingi lakini iwe kidogo.

Com. Ayonga: Asante, asante, Paul hiyo tumesikia.

Paul: Nikiongeza kidogo, kile kiko mimi mwenyewe ningependekeza serikali ichukue jukumu la kuangalia shule vile zilivyo, sababu shule kumekuwa na wanyanyasaji sana ningependelea shule ziingiliwe sana, sababu ziko na shida sana.

Com. Ayonga: Thank you so much could you please now go and register your name there. Now, katika wale niliokuwa nao hapa zamani nimewamaliza, thank you. Wale niokuwa nanyi hapa nimewamaliza hakuna ubaya chairman, could you please take your place. Na ambavyo chairman naona una memorandum kubwa kabisa tafadhali utupe summary ya maneno yako makubwa

makubwa na ikiwa kuna mengi hayo utupe tubebe. Go ahead.

Kilonzo: Thank you chairman of this sitting and the other Commissioners. My names are J.M.Kilonzo, John Mutuku Kilonzo. I will dwell on education, the presidency, agriculture, the police force and registration.

Ningetaka katiba ya leo ambayo tunaenda kuandikisha isimpe Rais atakaye kuwepo ruhusa ya kusimamia majeshi.

Number ya pili, ningetaka Rais atakayekuweko asikuwe head of universities lakini universities zisimamiwe na wale ambao wamekuwa ma-professionals wale wamehitimu katika eneo hili.

Ningependekeza kwamba wale ambao wamehitimu katika mambo kadha wa kadha wasimamie department zao politically. Ningeuliza pia katiba ambayo tunaendelea kutengeneza isimruhusu Rais atakayekuweko asimamie Judiciary. Ningetaka pia katiba itakayokuweko isimruhusu Rais a-appoint the most senior civil servants in this country wachaguliwe na Parliament.

Katika masomo ningeluliza education system iliyoko ya 8-4-4 ikuwe scrapped na tupewe ile system tulikuwa nayo zamani na badala ya kuwa na three semesters in one year tuwe na two semesters ili watoto wetu wawe na wakati wakutosha wa kupumzika. Ningependekeza kwamba katika katiba ijayo sheria itolewe ya kwamba watoto wakienda likizo iwe ni likizo lakini sio coaching.

Ningetaka wale waliotengeneza 8-4-4 system wakiwa na makusudi ya kuharibu watoto wetu wajaribiwe kotini kwa huu mpango kwa sababu haikutengenezwa na nia nzuri. Ningependekeza katika masomo pia watoto wote baada ya kumaliza form four walio na C plain and above, waruhusiwe kujiunga na vyo vikiu hata kama ni day scholars, kwa sababu C plain na kuendelea na juu ni mtu ambaye ametosha kupata shahada ya aina yoyote atakama ni ya doctorate ama lawyer ama whatever it is and profession. Wanafunzi wote wapewe loan kama itawezekana na walipe baada ya kumaliza chuo kikuu wale ambao wamepata C plain and above to create more lecture halls na tuandike more educationists in the universities badala ya kuzuia watoto wetu wasisome kwa sababu ya few facilities in our universities.

Kuhusu agriculture ningeomba mito yetu ambayo iko katika kila eneo la Kenya, we do what we call damming ili watu waweze kujitosheleza kwa chakula irrigation iwe provided tufungie mito mahali inawezekana halafu tu-improve our income by irrigating the wastelands which lies idle all the way to Mombasa from the highlands.

Kuhusu polisi, ningeomba polisi igawe mara kadha pamoja na the departments that are there ningeomba, number one, kitu ambacho kinaitwa medical police kiundwe katika nchi hii. Ilikuwa katika nchi ya South Africa na mtu wa kwanza, police wa kwanza kufika mahali kuna ajali ni medical police, kazi yao ni kuchukuwa wale ambao wameumia na kupeleka hospitalini. Ningeomba hio katiba ianzishe a department of medical police. Tukuwe na corruption police, tukuwe na traffic police, tuwe na

personal security police na criminal police. Pia ningeomba, askari wote ambo tuko nao ili tuondoe culture ya corruption in our police force na warudishe jina nzuri wawe retrenched tena na wapewe mishahara ambayo ni afadhali kidogo

Ile ingine ningesema kwa sababu kipande chetu, our ID card is only recognized in our villages and in our small towns ukifika katika airport utajua kile unabeba ni karatasi. Ningeomba kila mwananchi wa Kenya apewe passport badala ya kipande kwa sababu hii itatuwezesha kufanya kazi duniani kote na pili tukitoka nje ya nchi hii tutakuwa tuna weza kutambulikana.

Na ya mwisho ningeomba kwamba wale ambao wangetaka viti vya kila aina uBungena local government wasiruhusiwe kutumia pesa lakini watumie manifesto yao ambayo itaweza kutuambia watafanya nini katika nchi hii na character yao itumike kama viongozi wa kesho. Na iandikwe itakuwa ni hatia mtu kutumia pesa katika campaign atumie qualities zake na manifesto yake itusaidie. Thank so much unless there is a question.

Com. Ayonga: Huyu alikuwa Mr. John Mutuku Kilonzo ambaye ni chairman wa three Cs na bwana Kilonzo tunashukuru sana kwa hayo uliyoyasema na unaweza kutupa hiyo nini? Itakubidi uandike tena utupe kesho. Thank so much.

Kilonzo: Any question?

Com. Ayonga: It is very clear, it is straightforward. Kuna yeyote hapa ambaye amebaki kwa maana naona nimemaliza wale watu wangu nilio kuja nao na tafadhali usiongee just because unataka kuongea. Ongea kwa maana kuna point ambayo uliyotaka kusema ambayo haijasemwa. Usiongee tu kwamba watu walio kuja hapa waliongea uanze kurudia vile vile vilivyosemwa. Kama kuna jambo, una mzigo katika moyo wako na jambo hilo halijasemwa, unaweza kuja uliseme. Ni nani aliye na jambo linalomsukuma ambalo halijasemwa? Sasa nikiangalia nyinyi wawili naona huyu ni kama mzee, hebu muweke mikono yenu juu nione mzee, wewe unaangalia wapi mimi ninasema mikono. Ni hawa watatu, haya kuja mmoja wenu halafu mwingine afuate na mwingine afuate, keti kwa hicho kiti.

Bernard Mutiso: Mimi naitwa Bernard Mutiso. Ninataka kutoa mapendekezo yangu kuhusu hii sheria inatumiwa na local government, hii ya plot. Ukijenga plot yako na umenunua hiyo plot na ukajenga wewe mwenyewe na shida, mwisho unaona mtu mwingine anakuja kukuambia lazima uwe ukilipa hii plot. Hiyo sheria imepitishwa na wakoloni. Kwa hivyo ninaomba serikali yetu iondoe hiyo sheria.

Ingingine ni hii katiba inaturuhusu tuwe tukipatiwa title deeds na hiyo title deed niwe nikilipa na nikiendelea na kulipa nikimaliza miaka 97 hiyo kichaka lazima ni-renew kama mtu mgeni nchi hii. Kwa hivyo hiyo sheria inaonekana imepitishwa vibaya.

Com. Ayonga: Asante mzee, ya tatu.

Mutiso: Ya tatu, ni serikali yetu inataka kuondoa umaskini, lakini haitusaidii kwa hilo neno kwa sababu serikali kutoka mtu wa kwanza mpaka wa mwisho, huyu wa mwisho halipwi na huyu ni huyu mtu anaitwa mzee wa kijiji anaweza fanya kazi miaka mia na hapatiwi chochote na ni mtu anafanya kazi sana kwa hivyo sheria bado haijaangaliwa ilikuwa ni ile ile tu ilipitishwa na kikoloni. Kwa hivyo ninamba serikali yetu ikiwa inataka kumaliza umasikini nchi hii iangalie hiyo vitu viwili inaumiza mkaazi wa nchi hii akafanywa kama mgeni.

Com. Ayonga: Hebu mzee ngoja, enda kule ujiandikishe, yule mzee mwingine nimengoja, akapinga jinsi nilivyosema nilikuwa nalenga yule lakini umekuja endelea tu kijana

Alfonse Mutinda: My name is Alfonse Mutinda Kateti; I have only two things to suggest.

First is about the election. During Presidential elections I would suggest the leading candidate if he does not earn more than half of the total votes cast, we should have a second round whereby the leading candidate and number two they should go and people should vote again to select now the best out of the two.

Number two, is about land inheritance. There has been a lot of people not being not contented by the way people inherit the land especially in cases of polygamy. You find that it has been done in a traditional way, nowadays such that he let say a man has got two wives, the land is divided depending on the number of wives if they are two it is divided half way and you find that one of the wives might have only one child and another one has around ten and you see these ten children may start complaining because of the way the land has been divided. So I would rather suggest the Commission to come up with a clear way of dividing depending on the number of children but not the number of wives.

Com. Ayonga: Thank very much bwana Alfonse Kateti, unaweza kwenda kule ujiandikishe. Mzee sema majina yako.

Jacob Musyoki: Jina langu ninaitwa Jacob Musyoki Kilumba. Maoni yangu nazungumzia jambo moja tu uchaguzi wa county council. Maoni yangu ningependelea uchaguzi uendeleo namna ulivyo endelea hapo mbeleni. Huku watu (inaudible).....

Ingingine kitu nataka isiwe na mchanganyiko ni mayor, mayor mwenyewe achaguliwe na wananchi na wawe wakichaguliwa wawili kila sehemu, wakichagua mayor waende kwa ofisi ya council ili wachague mayor. Asichaguliwe na council peke yake.

Com. Ayonga: Asante sana mzee ulisema ulikuwa na oni moja tu. Asante sana unaweza kuenda kule ujiandikishe. You say you have one point, one point-one minute. And teacher you know there is summary and please summarise what is it that you forgot, we had already listened to her, I am just briefing other Commissioners.

Mary Nyawira: My name is Mary Nyawira, I did not forget you gave me three minutes instead of five, that is about the harambee. I think harambee, the fund Raisings in the country, they should be controlled because you find the President and Ministers and many other people they make contributions and if you look at those contributions versus their income you wonder where this money is coming from. So I think the money, they should control it in such a way that they know, let us say you are

told he gave one million today, he gave five hundred thousand, tomorrow I do not know he will have to be a multi-millionaire to give that kind of contributions. So I think they should check if he gives a contribution whoever it is at whatever level he should have indication from whom that money has been gotten, so that we control sometimes these fund Raisings we are bulldozed if it is an officer may be the divisional officer is having a fund Raising, he will force people to give him money. So I think they should control so that people are not bulldozed to give money and also these people who are contributing are not supposed to steal money so that their popularity is based on how much contribution they are giving, and also they should declare, if they are contributing more than their income they should declare where this money is coming from. Thank you.

Com. Ayonga: Thank you that was a nice ...

Interjection:

Com. Kangu: What is the best mechanism of controlling these people?

Mary: I have given two; one is to ensure that if somebody is contributing they are monitored because we get announcement even on the public media. If the contributions they make are above their income they should declare where the rest is coming from.

Com. Kangu: Why not just ask them for income tax on what is over and above and taxing?

Mary: That is what I am talking about, declaration so that we don't get these problems of bulldozing and also stealing to do that.

Com. Ayonga: Thank you now as chairman I want to stand and when I stand I am declaring something. I want to thank you all who have participated during the afternoon section and chairman wa hapa wa three Cs na bwana DO nadhani mumeona kwamba kila mmoja amesema mpaka ameishiwa and I want to thank you for your patience, I have seen many school children come in and come out because of the period I think they come during breaks and then they go back. I want to thank you for the very mature contribution you have made, what you have told us, what we have written in our notes and what we have recorded in the machine will not cheat and it will not skip anything. Even a small cough that you had it has been recorded that you coughed when you were giving your views. I want to now bring this meeting to a close I am sure the good Lord who helped us to come here has helped us to go through our programme. Is there anyone here who would volunteer to say a word of closing prayer before we leave? Mzee kuna microphone hapo,

From the crowd: tunawashukuru kwa kuja huku kwetu Ukambani.

